

RONALDO AMWAGA CHOZI URENO, UFARANSA ZIKIFUZU

UK. 21

Jumatano Julai 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581726

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Upandikizaji mimba sasa rasmi Muhimbili

UKURASA 2

**Nipashe** kinara habari za jinsia Afrika Mashariki

UKURASA 3


Nipashe

Mjamzito abakwa, afungwa katika kiroba

Kicheko kampuni za simu zikifuta tozo kutuma fedha

**Vifo** waandamanaji Kenya wafika 39, majeruhi ni 361



UKURASA 19

**Ongezeko** Kodi ya Majengo kwa Luku laibua jambo



UKURASA 5



UKURASA 7

**Mambo** manne yaliyoibeba TRA kukusanya trilioni 27.64/-

## Zitto ampigia simu Samia, akimjulia hali aliyetekwa

UK. 5



Kiongozi Mkuu mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, akimjulia hali Edgar Mwakabela, maarufu Sativa, katika Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam jana, anakopatiwa matibabu baada ya kutekwa na kuumizwa na watu wasiojulikana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mgeni wake, Rais wa Msumbiji, Filipe Jacinto Nyusi baada ya kuwasili katika viwanja vya Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Samia, Nyusi wakubaliana kuinua biashara iliyoporomoka

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAMLETEA MPINZANI AUCHO UK.24 **KATUNI** UK.6




Dk. Lisa Rusibamanyila (kushoto) kutoka Idara ya Magonjwa ya Dharura na Maafa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akifafanua jambo kwa mmoja wa watu waliotembelea Banda la MNH, katika Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa katika uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Rais Samia, Nyusi wakubaliana kuinua biashara iliyoporomoka

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS Samia Suluhu Hassan na mgeni wake, Rais wa Msumbiji Filipe Nyusi, wamesema biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili zimeshuka na kunahitajika ufufuaji wa haraka.

"Mwaka 2022 kiwango cha ufanyaji biashara kati ya Tanzania na Msumbiji kilikuwa Dola za Marekani milioni 57.8 lakini mwaka jana kilishuka hadi Dola za Marekani milioni 20.1," alitamka Rais Samia jana Ikulu jijini Dar es Salaam.

"Kwahiyo, tukaangalia nini kimesababisha anguko hilo. Tukakubaliana kushirikiana ili kuongeza," Rais Samia aliongeza wakati wakuu hao walipozungumza na waandishi wa habari baada ya mazungumzo yao ya faragha.

Rais alitaja maeneo 10 waliyokubaliana kushirikiana kiuchumi, yanajumuisha biashara, uwekezaji, sekta ya nishati, uchumi wa bluu, kilimo, ulinzi na usalama, sekta ya afya, miundombinu, ujenzi wa kituo cha forodha pamoja na kujumuisha ushirikiano huo na Afrika.

Rais Samia alisisitiza hali ya uwekezaji kati ya nchi hizo jirani si nzuri na ndiyo imejenga azma ya kuundwa ushirikiano huo, akitoa mfano, nchini kuna wawekezaji wawili tu kutoka Msumbiji huku Watanzania 16 ndiyo wamewekeza Msumbiji.

**"Nchi zetu zinapakana, hivyo tunapaswa kukuza uchumi. Kunapaswa kuwapo utafiti wa korosho, ili (zao) liweze kunufaisha zaidi mataifa yetu."**

"Namba hii ni ndogo, imetushtua hata sisi. Hivyo, tumekubaliana kuongeza. Katika wawekezaji hao wa Msumbiji waliopo hapa Tanzania wameleta ajira 650," alisema Rais Samia, huku akitaja mahususi wamekubaliana kuendeleza vyanzo vya nishati ya umeme kwa pamoja.

Alitaja eneo lingine ni kwenye uchumi wa bluu, hususani sekta ya gesi, akibainisha Msumbiji ina akiba ya gesi yenye ujazo metriki trilioni 100, huku Tanzania ikiwa na ujazo wa metriki trilioni 57.

Katika suala la masoko, Rais Samia alisema Tanzania na Msumbiji ni wazalishaji wa zao la korosho, lakini mamlaka ya upangaji bei zake iko katika soko la dunia.

Hivyo, akadokeza kuhusu mkakati wao wa kuvunja ngome ya upangaji bei ni kupitia azma yao ya kuunda umoja wa wazalishaji korosho Afrika utakaokuwa na sauti ya kuamua bei katika soko hilo.

Rais alisema wamekubaliana kushirikiana katika kuimarisha ulinzi na usalama mipakani, hususani kukomesha matukio ya kiharamia.

Hiyo inakwenda sambamba na kuboresha afya kwa wananchi wao, huku mwenza wake mkutanoni, Rais Nyusi, mwenyeji nchini na mweledi wa Kiswahili, akifafanua:

"Nchi zetu zinapakana, hivyo tunapaswa kukuza uchumi. Kunapaswa kuwapo utafiti wa korosho, ili (zao) liweze kunufaisha zaidi mataifa yetu."

Alihitimisha hoja yake, akigusia namna walivyonufaika katika mazungumzo yao, yakigusa mengi ya kimaendeleo baina yao, kwa upekee akigusa eneo alilolipa umuhimu, uimarishaji miundombinu.

# Upandikizaji mimba rasmi Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) itaanza rasmi upandikizaji mimba (IVF) Septemba mwaka huu, huku gharama kwa huduma hiyo ikiwa ni Sh. milioni 20.

Bingwa wa Masuala ya Kinamama Kitengo cha IVF MNH (Obstetrician and gynaecologist), Dk. Sabria Rashid, aliyesema hayo jana alipozungumza na Nipashe kwenye banda la hospitali hiyo katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya 48 Dar es Salaam (DITF).

Alisema kuwa kwenye maonesho hayo, kitengo hicho kimekuja na elimu kwa umma kuhusu huduma hiyo ambayo itaanza miezi miwili ijayo.

Bingwa huyo alisema kuwa wataanza na kundi la watu 10 kupewa huduma, akieleza kuwa gharama za upandikizaji ni kubwa kutokana na mahitaji ya dawa na vifaa ambavyo bei yake ni ghali.

"Mahitaji ya IVF ni makubwa. Tumewaona kliniki na wapo katika mchakato. Tukianza mwezi wa tisa (Septemba), tutaanza na hao ambao tutawasiliana nao. Unapozungumzia IVF siyo mwanamke tu, wapo wanaume ambao ni chanzo cha ugumba.

"Tukifanya uchunguzi na kugundua tatizo ni la baba, tutapandikiza mimba kwa mwanamke, lakini mbegu ya kiume kuchukuliwa pengine kwa mwanamume ambaye mbegu yake ni dhaifu. Jamii ijue utasa ni kwa jinsi zote," alisisitiza Dk. Sabria.

Bingwa huyo alisema wanaotafsiriwa kwamba ni wagumba ni walio kwenye uhusiano ama wanandoa waliopo pamoja kwa takribani mwaka mmoja na hushiriki tendo bila kufanikisha lengo lao la kupata mtoto.

Alisema ugumba upo wa aina mbili; waliopata mtoto na kukaa miaka kadhaa wakitafuta mtoto mwingine na ambao tangu kuzaliwa hawajawahi kushika ujauzito.

"Umri ukienda ni tatizo. Lakini tunapata pia walio katika umri wa kati. Kwa sasa kutokana na sababu za kimazingira, mabadiliko ya mtindo wa maisha kama vile watu wanatafuta elimu kwanza, kisha watoto.

"Utakuta umri unakwenda, kuja kuanza kutafuta mtoto tayari changamoto. Pia wapo vijana wadogo wameathiriwa na mazingira tofauti na zamani wenye umri mdogo hawakupata tatizo," alifafanua.

Bingwa huyo alisema uchunguzi hufanyika kabla ya IVF kwa jinsi zote. Huwa wanachunguza kwanza kubaini tatizo ndipo kuthibitisha haja ya upandikizaji.

Alisema uchunguzi huo hujumuisha pia kuangalia wanawake ambao mji wa mimba huiharibu mbegu ya kiume ikiwa safarini kwenda kwenye yai kutunga mimba.

Bingwa huyo pia alitaja wanaume kadhaa ambao mirija yao ina tatizo katika usafirishaji mbegu za kiume, hivyo hatua ya kuvuna mbegu hutumika.

"IVF mara nyingi tunashauri wajifungue kwa upasuaji kwa sababu gharama kubwa imetumika, hatua ndefu, tunapunguza hatari ya mtoto huyo kupitia uzazi wa asili," alisema.

Pia alisema upandikizaji hushauriwa uwe wa mtoto mmoja kutokana na kuchukuliwa tahadhari inayoweza kutokana na watoto pacha wawili au zaidi, kama vile kuzaliwa watoto njiti au ujauzito kuharibika.

Akifafanua unavyofanyika upandikizaji huo, bingwa huyo alisema: "Kwanza, mayai kadhaa hupevushwa, labda mayai 10 na kuwa embrio, katika watoto 10 hatuwezi kukupandiza wote, tutahifadhi embrio (kiini tete).

"Ikitokea utahitaji tena baada ya miaka miwili utakuja, au ikitokea dharura ujauzito umetoka tutakuwekea mimba nyingine.

"Ila kuna gharama ya kuhifadhi embrio kwa ambao watahitaji huduma hiyo, labda wanakwenda kutafuta kwanza maisha, baadaye wanakuja kupandikiza."

Kuhusu muda unaofaa kuanza mzunguko mpya wa IVF baada ya mzunguko wa awali ambao haukufanikiwa, bingwa huyo alisema ni baada ya mapumziko ya miezi miwili hadi mitatu.

"Hakuna kikomo cha umri ingawa hali ya afya itatumika kufahamu kama mtu anaweza kupokea matibabu. Uwezekano wa kupata mimba hupungua kadri umri unavyosonga. Inachukua muda wa mwezi mmoja na nusu, ili kukamilisha mzunguko wa IVF.

"Hii inajumuisha udhibiti wa homoni, sindano za kuchochea uzalishaji mayai na utaratibu kamili wa maabara ya IVF," alifafanua bingwa huyo.

HABARI KITAIFA

# Nipashe namba moja uandishi habari za jinsia, jumuishi

**Na Grace Mwakalinga**

GAZETI la Nipashe limeshika nafasi ya kwanza nchini kwa weledi wa kuandika habari zinazohusu masuala ya wanawake huku likiwa namba tano katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki.

Taarifa hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mwananchi Communications Ltd, Bakari Machumu wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari na wakufunzi wa masuala ya jinsia na mawasiliano yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Agha Khan Graduate School of Media and Communications

Alisema matokeo hayo yametolewa kutokana na ripoti ya 'State of Media reporting in East Africa' kwa kuhusisha vyombo mbalimbali vya habari ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema ripoti hiyo inafafanua kuwa gazeti la Nipashe limeandika mada 225 zinazohusu masuala ya wanawake na kufikisha asilimia 20, huku gazeti la Daily Nation la nchini Kenya likiandika mada 306 na kufikisha asilimia 24.

"Gazeti la Nipashe ndilo namba moja hapa nchini kwa kuandika habari zinazohusu masuala ya wanawake kwa asilimia 20 likifuatiwa na Mwananchi ambalo limeandika kwa asilimia tisa, tunawapongeza kwa jitihada hizo naamini na vyombo vingine vya habari vitaendelea kuandika ili kuwapa nafasi wanawake," alisema Machumu.

Kwa mujibu wa Machumu, Nipashe pia linafanya vizuri kidijitali kuandika habari za wanawake kwa ukanda wa Afrika Mashariki na limekuwa namba nne huku likiwa nafasi ya kwanza Tanzania likipiku vyombo vingine vya kidijitali.

Alifafanua kuwa habari za wanawake zinazoandikwa zaidi zinahusu matukio, zikifuatiwa na masuala ya siasa, uchumi, biashara, utamaduni na dini.

"Masuala ya kijinsia sio masuala ya wanawake pekee. Napenda kusema kuwa kuripoti na kuwa na uwiano kuhusu masuala ya kijinsia ni vizuri kwa biashara kwenye vyombo vyetu vya habari nchini."

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Agha Khan kitivo cha Shule ya Uzamili wa Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma, Prof. Nancy Booker, wakati akizindua ripoti hiyo alisema kuwa katika utafiti huo gazeti la Nipashe limekuwa kinara kwa kuzingatia masuala ya jinsia zote katika uandishi wake.

Utafiti huo ulifanywa mwaka 2023 Juni hadi Desemba kwa kuhusisha vyombo vikubwa vya habari katika nchi za Afrika Mashariki 19 na Nipashe kuibuka kinara katika kuandika masuala ya wanawake na kuzingatia usawa wa jinsia.

"Katika uandishi wake Nipashe iliweza kuzingatia masuala ya wanawake na imefanya jitihada wanawake kujulikana na sauti zao kusikika zaidi," alisema Prof. Nancy.

Prof. Nancy alitoa wito kwa vyombo vingine vya habari nchini kuiga mfano wa Nipashe kwa kuwa kwa sasa dunia nzima haina masuala ya jinsia na kuvitaka kuandika kwa kuzingatia usawa.

"Masuala ya jinsia yamekuwa mtambuka ulimwenguni mbadiliko ya sayansi na teknolojia yamechangia kuongeza ujuzi wa mambo, hivyo ni vyema vyombo vya habari kuandika habari kwa kuhusisha vyanzo mbalimbali vya habari ili kutoa nafasi kwa jinsia zote na kusaidia kundi la wanawake kufanya maamuzi ndani ya vyombo vya habari," aliongeza Prof. Nancy.

KLINIKI YA MAKONDA

# Tabibu ashauri mwalimu aliyeugua arejeshwe kazini

**Na Beatrice Shayo, ARUSHA**

KAMBI maalum ya madaktari bingwa iliyokuwa inatoa huduma bure mkoani Arusha imebaini mwalimu aliyeacha kazi ya ualimu alikuwa anakabiliwa na tatizo la afya ya akili na uongozi wa mkoa umeombwa kumsaidia arudishwe kazini.

Hayo yalisemwa juzi jioni na Msaikolojia Tiba wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Alex Ndagabwene, wakati akitoa tathmini ya wagonjwa aliohudumia katika kambi hiyo iliyodumu kwa siku nane kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Ndagabwene alisema kuna kesi ya afya ya akili ambayo ilimpata mwalimu ambaye tangu mwaka 2016 alikuwa anapatiwa matibabu bila kutoa taarifa kazini.

"Baadaye anapotea, anakaa nyumbani hadi mwaka ama miwili ndipo anarudi kazini, sasa amejikuta hawezi kupatiwa mshahara wake kwa sababu ameshatolewa kwenye malipo.

"Sisi tumeona changamoto hii kwa sababu alianza kuumwa ugonjwa wa afya ya akili akiwa kazini, alivyorudi nyumbani akawaeleza hawezi kuendelea na kazi kwa kuwa aliona watu wanamtisha kazini na wengine kuwaona ni wabaya ofisini, huu ugonjwa ndivyo unavyoanza," alisema.

Aliongeza kuwa ugonjwa huo una tabia hiyo ya mtu kuacha kazi ndani ya saa 24 au 48 na kuondoka bila kuacha taarifa yoyote kwa kuwa ugonjwa unakuwa umeanza.

Alisema kuwa asipotokea mtu kumfuatilia anaweza asionekane ofisini hadi miaka mitatu ama kuacha chuo bila kutoa taarifa kutokana na shida ya ugonjwa wa afya ya akili.

"Tunaomba uongozi wa mkoa kumsaidia mwalimu huyu arudi kazini kwa kufuata taratibu zinazohitajika, tutashukuru sana," alisema.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Ndoto ya MSD kuzalisha vifaa tiba nchini yatimia

**Na Restuta James,**
NJOMBE

NDOTO ya upatikanaji wa uhakika wa vifaa tiba nchini iko mbioni kutimia baada ya Bohari ya Dawa (MSD) kuanza kuzalisha mipira ya mikononi (gloves) katika kiwanda chake cha Idofi kilichoko Halmashauri ya Mji wa Makambako, mkoani hapa.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari waliotembelea kiwanda hicho jana, Kaimu Meneja wa kiwanda hicho, Shiwa Mushi, alisema uzalishaji rasmi ulianza Februari mwaka huu na tayari wameshatengeneza mipira jozi milioni mbili.

Alisema wanatarajia kuzalisha mipira hiyo jozi milioni 86.4 kwa mwaka ambayo itakidhi mahitaji ya ndani kwa asilimia 83.4 kwa muda huo.

Mushi alisema kwa sasa wanazalisha mipira inayovaliwa na watoa huduma za afya wanapomfanyia mgonjwa uchunguzi (examination) na kwamba kiwanda kitaanza kuzalisha mipira ya watoahuduma wanaofanya upasuaji hivi karibuni.

"Kama mlivyoona, kazi yote ya uzalishaji inafanyika kwa umakini na kuzingatia ubora katika kila hatua kwa sababu bidhaa za afya zinahitaji usafi wa hali ya juu. Tunazingatia vigezo vya ubora kama tulivyoelekezwa na mamlaka za udhibiti," alisema.

Kwa mujibu wa meneja huyo, mahitaji ya mipira hiyo nchini ni jozi milioni 104, hivyo uzalishaji huo utaokoa zaidi ya Sh. bilioni 20 zilizokuwa zinatumiwa na serikali kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

Alisema hadi sasa serikali imeshatumia Sh. bilioni 10 kujenga na kununua mitambo ya uzalishaji kiwandani huko.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa MSD, Etty Kusiluka, alisema bohari hiyo ina viwanda vitano. Kati yake, vitatu vinafanya kazi na viwili viko mbioni kuanza uzalishaji.

Alisema viwanda vinavyotarajiwa kuanza uzalishaji wakati wowote ni cha bidhaa za pamba kilichoko Simiyu na cha dawa mbalimbali kilichoko eneo la Zegereni, mkoani Pwani.

"Baada ya maboresho ya sheria, MSD sasa ina majukumu manne ambayo ni kuzalisha, kununua, kutunza na kusambaza dawa na vifaa tiba nchini. Ili kufanya kazi kwa ufanisi, hivi karibuni Waziri wa Afya alizindua kampuni tanzu ya MSD itakayosimamia viwanda vyote vilivyopo chini ya bohari," alisema.

Takwimu za Wizara ya Afya zilizotolewa na waziri wake hivi karibuni, zinaonesha kwamba asilimia 85 ya bidhaa za afya, zikiwamo dawa, gloves na vitendanishi, zinanunuliwa nje ya nchi na kwamba lengo la serikali kuanzisha viwanda hivyo ni kuhakikisha upatikanaji bidhaa hizo kwa asilimia 50.

# Stempu za kielektroniki zaja kwenye saruji, sukari

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) iko katika mchakato wa mwisho wa kuweka stempu za kielektroniki (ETS) kwenye sukari na saruji ili kupunguza matukio ya ukwepaji kodi na kughushi.

Akizungumza katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) ambayo yanafanyika kila mwaka na kuandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Mambo ya Ndani wa TRA, Ndositwe Haonga alisema hatua hiyo itasaidia walaji kununua bidhaa asilia kutoka kwa wazalishaji.

Uanzishwaji unaotarajiwa wa stempu hizo za kidijiti kwa saruji na sukari ni baada ya kufanikiwa katika sigara, bia, mvinyo, vinywaji vikali na maji ya chupa ulioanza kutumika Januari 15 mwaka jana.

Haonga pia alisema hatua hiyo itasaidia TRA kukusanya ushuru zaidi utakaosaidia nchi kuboresha miradi ya maendeleo.

Awali Ofisa Mwandamizi wa Usimamizi wa Kodi TRA, Patric Massawe alitoa wito kwa Watanzania kutumia mfumo wa 'Hakiki Stempu' kwa ajili ya kupata bidhaa halisi na zenye ubora wa viwango.

Alisema kuwa watu wenye mfumo huo watakuwa na uwezo wa kukagua kujua kama bidhaa wanazonunua ni halisi na viwango kwa kulinda afya yao.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mashimba Ndaki, alipendekeza stempu za kidijiti zitumike kwenye bidhaa nyinginezo kama vile saruji na sukari.

"Taratibu zinaendelea kwa kikao kati ya kamati na serikali kupitia TRA ili kupendekeza namna ya uwekaji stempu za kidijitali kwa bidhaa tajwa hapo juu na nyinginezo ili kuongeza ukusanyaji mapato.

"Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa stempu za kielektroniki zimekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza ushuru kwa serikali na hivyo zinapaswa kusambazwa kwa bidhaa nyingine ili kupunguza mianya ya ukwepaji kodi na kutangazwa kwa bidhaa zinazozalishwa," alisema.








# Zitto ampigia simu Samia, akimjulia hali aliyetekwa

**Na Halfani Chusi**

ALIYEKUWA Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe amekwenda hospitalini kumjulia hali Edgar Mwakabela, maarufu Sativa, aliyetekwa Dar es Salaam na kuteswa kisha kutelekezwa porini mkoani Katavi.

Zitto pia amesema ameshampigia simu Rais Samia Suluhu Hassan kumshauri ufanyike uchunguzi wa kina kuhusu tukio hilo ili wahusika wote wachukuliwe hatua za kisheria.

Mwanasiasa huyo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akiwa nje ya hospitali alikolazwa kijana huyo.

Alisema kuwa baada ya kuona taarifa za kijana huyo kupitia mitandao ya kijamii, juzi alimtafuta Rais Samia na kuzungumza naye kuhusu tukio hilo la kutekwa, kupigwa risasi na kutupwa msituni mkoani Katavi pamoja na matukio mengine ya watu kupotea.

Zitto alisema aliamua kumweleza masuala hayo Mkuu wa Nchi kwa kuwa ana wajibu wa kulinda usalama wa raia huku akimsisitizia kuwa matukio ya namna hiyo yanachafua taswira, haiba yake na yanaondoa maana halisi ya falsafa yake ya R4.

"Rais alinisikiliza na ameahidi kufanyia kazi ushauri wangu, na kwa hatua ya awali amenieleza kuwa yeye binafsi atabeba gharama zote za matibabu ya Sativa kuanzia sasa mpaka atakapopona kabisa pamoja na kuhakikisha unafanyika uchunguzi wa tukio hilo.

"Ninamshukuru kwa mwanzo wake mzuri. Kila safari ndefu inaanza na hatua ya kwanza, ninaamini sasa tumeanza safari ya kwenda kule tunakotaka ambako tabia za kutesana zitakomeshwa," alisema Zitto.

Alisema matukio ya utekaji yanaharibu taswira na kuirudisha nchi katika zama ambazo anaamini ilishatoka, hivyo njia pekee ya kukomesha vitendo hivyo ni uchunguzi huru wa kina au wa kijaji kusaidia kukomesha matukio hayo.

Zitto pia alishukuru wananchi waliotumia mitandao ya kijamii kupaza sauti bila kujali itikadi za kisiasa, hata kufanikisha Sativa kupatikana.

Mwanasiasa huyo alisema kuwa ndivyo vijana wanavyopaswa kuwa pamoja na kuhakikisha wanashiriki kukomesha matukio ya aina hiyo.

Sativa, mkazi wa Mbezi, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, alipatikana Juni 27 mwaka huu mkoani Katavi, akiwa na majeraha mwilini, akiomba msaada wa kupelekwa hospitalini.

Watanzania wengine waliowahi kutekwa nchini ni pamoja na: Mwanaharakati Mdude Nyagali, msanii Roma Mkatoliki, Bilionea Mohamed Dewji 'Mo' na Raphael Ongangi.

Pia kuna orodha ya wanaodaiwa walitekwa na hawakupatikana mpaka leo, ikijumuisha majina ya Ben Saanane, Azory Gwanda na Simon Kanguye.




Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Abdul-Razaq Badru (kulia), akimhudumia mwanachama wa mfuko huo, Sikudhani Semka kwenye banda la mfuko huo, katika maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TANESCO yatoa ufafanuzi madai ongezeko Kodi ya Majengo kwa Luku

**Na Jenifer Gilla**

MJADALA wa kulalamikia ongezeko la kodi ya majengo inayokatwa kwenye malipo ya Luku umeliibua Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) na kutoa ufafanuzi.

Malalamiko ya wateja walionunua umeme na kiwango walichopata yalitawala kwenye mitandao ya kijami jana kuhusu tofauti hiyo.

Malalamiko hayo ni makato ya Sh. 2,000 badala ya Sh.1,500 ya kodi ya majengo wanaponunua umeme wa Luku bila kupewa taarifa kutoka kwa mamlaka husika.

TANESCO ililazimika kutoa ufafanuzi huo kuwa hakuna ongezeko lolote lililofanyika kwenye viwango vya kodi ya majengo isipokua kinachokatwa ni madeni ya nyuma yaliyotakiwa kulipwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Fadhila Hussein, mkazi wa Tabata alilalamika kukatwa kiasi hicho cha fedha baada ya kununua umeme wa Sh. 25,000 juzi bila ya kupata taarifa yoyote ya ongezeko la kodi ya majengo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wala TANESCO.

"Nashangaa kuona nimekatwa Sh. 2,000 wakati najua kodi ile ni Sh.1,500, na nimefuatilia Bunge sijaona wakizungumzia ongezeko la kodi ya majengo, sasa najiuliza hili ongezeko limetoka wapi," alihoji Fadhila.

> **"Nashangaa kuona nimekatwa Sh. 2,000 wakati najua kodi ile ni Sh.1,500, na nimefuatilia Bunge sijaona wakizungumzia ongezeko la kodi ya majengo, sasa najiuliza hili ongezeko limetoka wapi," alihoji Fadhila.**

Joseph Daudi, mkazi wa Temeke alisema alikatwa kiasi hicho jana na kulalamika kuwa kitendo cha serikali kuongeza gharama hizo bila kuwapa taarifa sio cha kiungwana.

Msemaji wa Shirika hilo, Kenneth Boymanda, alisema hakuna ongezeko la kodi ya jengo isipokuwa Sh. 500 iliyoongezeka katika kodi hiyo ni fedha iliyotakiwa kukatwa mteja tangu Julai, mwaka jana.

Alisema, baada ya serikali kutangaza mabadiliko ya viwango vya kodi ya majengo kwa mwaka wa fedha 2023/24, makato yalitakiwa yaongezeke kuanzia Julai mosi, 2023 kutoka Sh.1,000 hadi Sh. 1,500.

Alisema, wateja walionunua umeme kuanzia Julai mosi hadi 25 walilipa kiwango cha zamani cha Sh.1,000 badala ya kipya cha Sh.1,500 na kubaki na deni la Sh. 500. Aidha, mteja aliyetakiwa kulipa Sh.7,500 alikatwa Sh.5,000 ya zamani na kuwa na deni la Sh. 2,500.

"Kwa kuwa madeni ya fedha hizo hayakulipwa kwa baadhi ya wateja kinachotokea kwa sasa kuanzia Juni mosi, 2014 ambao ni mwaka wa fedha mpya wa 2024/2025 ni kwa mteja kukatwa kiwango ambacho hakikulipwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024," alisema.

Taarifa kwa umma iliyotolewa na Shirika hilo jana ilifafanua kuwa makato ya madeni hayo yatafanyika mara moja na yanatakiwa kulipwa kwa pamoja wakati mteja akifanya ununuzi wa umeme kwa mara ya kwanza kuanzia Julai 2024.

Shirika lilifafanua kuwa baada ya hapo mteja ataendelea kulipia viwango vya kawaida kulingana na aina ya nyumba anayoishi kama mwongozo wa TRA Julai 26, 2023 unavyoelekeza, Sh. 1,500 kwa nyumba ambayo sio ya ghorofa na Sh.7,500 kwa sakafu moja ya nyumba ya ghorofa kila mwezi.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, Meneja wa Elimu kwa Mlipa Kodi TRA, Paul Walalaze alisema, mamlaka hiyo haihusiki na ukusanyaji wa kodi za majengo kwa kuwa suala hilo lilihamishiwa kwenye halmashauri, manispaa na majiji.

Julai 26, mwaka jana TRA kwa kushirikiana na TANESCO iliutaarifu umma kuhusu mabadiliko ya viwango vya utozwaji uliotokana na mabadiliko ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji Kodi ya Majengo Sura ya 289 kupitia Sheria ya Fedha ya 2023.

Ilisema kutokana na mabadiliko hayo, nyumba ya kawaida iliyokuwa ikitozwa Sh.12,000 kwa mwaka itatozwa Sh.18,000 sawa na Sh. 1,500 kwa mwezi, huku nyumba za ghorofa katika maeneo ya majiji, manispaa na halmashauri za mji zilizokuwa zinatozwa Sh. 60,000 kwa kila sakafu zitatozwa Sh. 90,000 sawa na Sh. 7,500 kwa mwezi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapambano dawa za kulevya elimu ianzie shuleni

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya hasa kwa vijana yameathiri nguvu kazi na kusababisha wengi wao kuishia mitaani na kufanya vitendo vya uporaji ili wapate pesa ya kununulia dawa hizo.

Wazazi wamekuwa katika wakati mgumu hasa baada ya kujitoa kuwasomesha vijana wao na kinyume walivyotarajia kuwa watakuwa msaada, wanageuka kuwa mzigo kwa familia.

Wengi wa vijana hao wanaharibika kutokana na makundi wanayoambatana nao na kupata vishawishi vya kutumia dawa hizo.

Baadhi ya wazazi wanatumia gharama kubwa kuwasomesha watoto wao nje ya nchi, lakini wakirudi nchini tayari wamesha athirika na dawa za kulevya.

Kutokana na tatizo hilo, serikali imeamua kuchukua hatua ili kudhibiti kikamilifu matumizi ya dawa za kulevya nchini, kwa kupanga kuhamishia elimu inayoendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali, kuipeleka kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu kama ilivyo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa jijini Mwanza katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya kupiga vita dawa za kulevya duniani alisema "ni lazima tuimarishe mikakati yetu ya kukabiliana na mapambano haya na serikali imejikita katika kutoa elimu ili jamii ifahamu na tutakwenda kuanzisha klabu katika shule za Msingi, Sekondari mpaka Vyuo Vikuu kama walivyofanya TAKUKURU ili kupunguza kama si kumaliza kabisa tatizo hili."

Pia, vijana wa kitanzania wametakiwa kuachana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya na badala yake waungane katika kufanya shughuli halali za kiuchumi ili wajiletee maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na hata taifa.

Kadhalika, jamii inatakiwa kuelimishwa zaidi kuhusu athari za matumizi ya dawa hizo na kuwa njia hiyo itakuwa mwarobaini wa tatizo hilo sugu pamoja na kuwawezesha waliotoka kwenye uraibu (waraibu) ili waweze kujumuika na wenzao wafanye kazi na waweze kujisimamia.

Kuhusu taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, ya hali ya dawa za kulevya katika Mkoa wa Mwanza kuanzia mwaka 2018 hadi 2023, wananchi waliopatikana na bangi ni 1,797, mirungi 294, dawa za kulevya (cocaine, heroin na nyingine) 51 na kufanya jumla ya dawa zote kuwa 2,142.

Takwimu hizi zinabainisha kwamba biashara na matumizi ya dawa za kulevya mkoani Mwanza ni kubwa na inahitaji msukumo mkubwa kutoka kwa serikali pamoja na wadau mbalimbali ili kuendelea kupambana na wazalishaji, wasambaji na watumiaji wa dawa hizo.


Ukiangalia vijana wengi wanao athirika ni kutoka katika majiji ambako hufanyika mambo mengi ya starehe na hupata vishawishi vya kujiingiza kwenye matumizi hayo kama sehemu ya starehe.

Vijana wanao athirika ni wa jinsi zote na kusababisha wazazi wengine kupata msongo wa mawazo kutokana na hali wanayopitia kwasababu wengine hugeuka wezi kwenye nyumba zao ili wapate pesa za kuwawezesha kununua dawa hizo.

Vita ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa kwasababu inahusisha wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo kipesa ambao wanaweza kutumia nguvu yao ya pesa kuendeleza biashara hiyo.

Jambo la muhimu kabisa ni elimu kwa vijana hasa katika shule ambako wengi hushawishiwa kutokana na uelewa wao mdogo wa kufahamu lipi zuri na lipi baya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Usikwepe siasa ndiyo inayoamua hatima

**BAADHI** ya watu wanasema; "siasa tuwaachie wanasiasa tutafute pesa kujikwamua kimaisha, hatima ya maisha yako iko mikononi mwako, lakini wanasahau kuwa siasa ni maisha haikwepeki.

Ni kwa sababu viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, mtaa, kata, majimbo na taifa, wanatokana na siasa, ndiyo wanaoamua mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo na maisha ya wananchi akiwamo anayesema anawaachia wanasiasa.

Kimsingi, siasa ndiyo hupanga bei za bidhaa mbalimbali na suala la kupanda au kushuka kwa kodi, kwa sababu wahusika wakuu kwenye maamuzi ni wabunge na mawaziri wanaoiwasilisha ,kuijadili na kuipitisha bajeti.

Wanatokana na siasa, kwa sababu wanachaguliwa kupitia sanduku la kura. Hivyo, ni muhimu kila mwenye sifa za kupiga kura akajihusisha na siasa, kuchagua viongozi bora kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Iwapo watu wataendelea kujitenga na siasa, wakidhani kuwa haiwahusu, inaweza kuwa wakachaguliwa kupatikana viongozi ambao si sahihi, watakaokwamisha maendeleo, kwa kukosa uwezo wa kuongoza.

Umuhimu wa kila Mtanzania mwenye sifa kushiriki kwenye uchaguzi, ndio ambao unaifanya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kuboresha daftari la kudumu la wapigakura.

Daftari linaboreshwa, ili kila aliyefikisha umri wa miaka 18 aweze kuandikishwa, hatimaye ashiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kupata viongozi watakaoongoza nchi kwa miaka mitano ijayo.

Julai 20 mwaka huu, kazi ya uboreshaji wa daftari hilo, inatarajiwa kuanza mkoani Kigoma kwa muda wa siku saba, kisha mikoa mingine huku tume ikitumia muda wa siku saba kwa kila mkoa.

Kila mara tume imekuwa ikihimiza watu akujiandaa kujiandikisha au kuboresha taarifa zao, kwani inajua inajua umuhimu wa Mtanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 kushiriki uchaguzi huo.

Tume inatambua kuwa siasa ni njia ya kufanya maamuzi katika ngazi mbalimbali, kwani katika demokrasia, kila mtu ana kiasi fulani cha nguvu, kwa hiyo siasa ya demokrasia watu wote huchangia maamuzi.

Ninadhani si sahihi kutojiingiza katika siasa siasa halafu watu wengine wanapochagua viongozi ambao labda hawawezi kuongoza, waanza kulaumu wanasiasa na kumbe wao ndio wamechangia hali hiyo.

Kushiriki katika uchaguzi kwa kuchagua viongozi ni jambo sahihi, lakini kujiweka pembeni, kwa maelezo kuwa hawataki kujiingiza katika siasa, kunaweza kuchangia kupata viongozi wasiofaa.

Hivyo, ingefaa kila mmoja kutafakari na kisha kuchukua hatua za kushiriki katika uchaguzi, kwa kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura au kuboresha taarifa kwa wakati.

Ingekuwa ni vyema wakati daftari halijafika mkoani kwetu, tujipange kufika kwenye vituo vya kujiandikisha ili kutoa taarifa sahihi na kupata kadi na kujiandaa kushiriki kwenye uchaguzi ujao.

Lakini pia wakati tume inajipanga kuboresha daftari hilo, ni vyema kukumbuka kuwa mwaka huu kuna uchaguzi wa viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa, wenye kadi za kupigia kura wasijiweke pembeni.

Kwa nini? Kwa sababu wapo baadhi ya watu ambao wamekata tamaa baada ya kupigia kura wagombea wao, lakini baada ya matokeo kutangazwa, wakawa wameshindwa.

Baadhi yao husema, hawataki kushiriki uchaguzi, kwa maelezo kwamba hata wakipiga kura, watachaguliwa wengine, hivyo wanaona ni bora wawaachie wachache masuala ya siasa au uchaguzi.

Ikumbukwe kuwa wanaojiweka pembeni, maana kwamba wataendelea kuchaguliwa viongozi na wenzao ambao si chaguo lao. Hivyo, njia nzuri ni kushiriki uchaguzi bila kuacha hadi kieleweke.

Tusikwepe siasa, tujiandae kujiandikisha na kuboresha taarifa zetu, lakini pia tukumbuke kuwa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa uko mlangoni, tujipange kuchagua viongozi makini.

## BoT: Zuio la matumizi ya Dola litaongeza thamani ya Shilingi

**Christina Mwakangale na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema kuzuiliwa matumizi ya Dola kwa taasisi mbalimbali nchini kutasaidia kuleta ahueni na kuongeza thamani ya Shilingi.

Mchumi kutoka Idara ya Sera za Fedha BoT, Marwa Patrick, aliyasema hayo jana, alipozungumza waandishi wa Nipashe kwenye banda la benki hiyo katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya ya 48 Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba, yanayoendelea mkoani humo.

"Tunaamini ni hatua nzuri ambayo itasaidia kupunguza presha inayoonekana pamoja na kuimarika kwa Shilingi yetu, kwa sababu sekta za serikali nazo zilikuwa zinahitaji Dola.

"Mfano mtu amefanya kosa anahitaji kulipa faini, alikuwa analazimika kuingia sokoni kutafuta Dola ili alipe. Kwahiyo, tunaamini kuzuiliwa kwa matumizi ya Dola au kupokea, kutasaidia ahueni ya Shilingi yetu kuwa imara," alisema Marwa.

Ofisa huyo wa BoT alisema pamoja na hatua hiyo, kuna akiba ya kutosha ya Dola nchini inayotosheleza matumizi ya zaidi ya miezi minne na nusu kama ambavyo Gavana wa BoT amekuwa anasisitiza, ikiwamo taarifa yake ya mwezi Aprili mwaka huu.

"Kwahiyo, hata wawekezaji wanaoagiza au watu wanaohitaji kwa ajili ya matumizi ya Dola tunawapa uhakika kwamba wawe na imani fedha za kigeni zipo na BoT imejizatiti kabisa katika hilo," alifafanua Marwa.

"Ukizingatia kwamba sasa hivi tunakwenda katika kipindi cha 'high season' kwenye mapato ya utalii ambacho watu wengi wanatoka kwenye mataifa mbalimbali kuja kupumzika Tanzania, tunategemea kupata fedha nyingi kutoka vyanzo tofauti vya utalii.

"Na Tanzania inakwenda kipindi cha kuuza mazao yake ya asili nchi za nje, hii yote inatoa mwanya wa kuwahahakikishia Watazania kwamba wasiwe na shaka, Shilingi itaendelea kuimarika," alisema Marwa.

Alisema kuwa Julai Mosi, mwaka huu, Dola mojaya Marekani ilikuwa inabadilishwa kwa Sh. 2,620 na BoT inaamini kwamba hali hiyo itaendelea kuwa nzuri.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati akiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka huu wa fedha (2024/25), aliagiza ifikapo Julai Mosi, taasisi za umma nchini zinazofanya shughuli za kupokea fedha ya kigeni, kuanza kutumia Shilingi ya Tanzania.

Tayari baadhi ya taasisi kama vile Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) zimeanza kufanya mabadiliko ya malipo kwa viwango vya Dola na kuwa kwa Shilingi.




Mhitimu wa Chuo cha Ufundi Stadi VETA Mkoa wa Arusha, George Nyahende, akionyesha mashine aliyobuni mwenyewe ya kutunza watoto wanaozaliwa kabla ya muda wao yaani njiti, wakati wa maonyesho ya 48 biashara ya kimataifa yanayoendelea katika uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mambo manne yaliyoibeba TRA kukusanya trilioni 27.64/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetangaza ilikusanya Sh. trilioni 27.64 kwa mwaka uliopita wa fedha (2023/24).

Kwa mujibu wa Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, makusanyo hayo sawa na ufanisi wa asilimia 97.67 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 28.30.

Makusanyo haya pia ni ongezeko la asilimia 14.50 kulinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 24.14 katika mwaka wa fedha 2022/23.

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2023/24, (Aprili - Juni, 2024), TRA imefanikiwa kukusanya Sh. trilioni 7.09 sawa na ufanisi wa asilimia 99.46 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 7.13.

"Makusanyo haya ni ongezeko la asilimia 24 kulinganisha na kiasi cha Sh. trilioni 5.72 kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23," alisema Kidata katika taarifa yake kwa vyombo vya habari juzi.

Kwa mujibu wa Kamishna Mkuu Kidata, ongezeko hilo la makusanyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 limechagizwa na mambo makuu manne ambayo ni pamoja na ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini hususani uzalishaji viwandani na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea nchini kujionea vivutio mbalimbali vilivyopo.

Kidata alitaja jambo la pili ni mwitikio mzuri wa walipakodi wengi katika kuwasilisha ritani na kulipa kodi kwa wakati.

Jambo la tatu kwa mujibu wa Kamishna Mkuu huyo ni kuongezeka kwa uhiari wa ulipaji kodi kufuatia maboresho yanayoendelea kufanywa na TRA ikiwamo uboreshaji mifumo ya TEHAMA, kusogeza huduma jirani na walipakodi kwa kuanzisha Divisheni za Walipakodi Wadogo na Walipakodi wa Kati pamoja na kuendelea kusuluhisha pingamizi za kodi nje ya mahakama.

Kidata alisema jambo la nne ni kuongezeka uingizwaji wa mizigo toka nje ya nchi kutokana na uboreshwaji wa mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

Pamoja na mafanikio haya, Kidata alisema vitendo vya ukwepaji kodi na kutozingatia sheria vimeendelea kushamiri miongoni mwa makundi mbalimbali ya walipakodi ikiwamo watu binafsi, kampuni za ndani na yale ya kimataifa.

Alisema TRA itaendelea kuhimiza ulipaji kodi kwa kufuata sheria zilizopo na utekelezaji wake kuzingatia misingi ya utawala bora.

Kidata pia alisema TRA inaendelea kuhimiza matumizi ya njia ya majadiliano na maridhiano katika kuzuia na kutatua migogoro mbalimbali ya kikodi kwa kuwa mara nyingi njia hiyo imekuwa ikileta matokeo chanya yenye manufaa kwa pande zote.

"Hata hivyo, inapojitokeza migogoro isiyoweza kumalizwa kwa njia ya majadiliano, TRA inahimiza walipakodi kutumia haki yao ya kisheria kwa kufuata utaratibu wa kushughulikia mapingamizi na rufani za kodi uliopo kwa mujibu wa sheria hususani kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 na Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408.

"Utaratibu huu utahakikisha migogoro ya kodi inatatuliwa kwa kufuata misingi ya sheria na haki kupatikana bila kuleta taharuki kwa jamii.

"TRA inapenda kuwashukuru walipakodi na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kulipa kodi ikiwa ni njia muhimu ya kuunga mkono juhudi za kuleta maendeleo nchini zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania," alisema Kidata katika taarifa yake hiyo.


Katika kuendeleza hilo kwa vitendo, Kamishna Mkuu huyo alisema TRA inaendelea kutoa wito kwa walipakodi na wananchi wote kuendelea kutoa na kudai risiti za Kielektroniki (EFD) kwa kila ununuzi wa bidhaa au huduma, kuhakiki uhalali wa stempu za kielektroniki za kodi (ETS) katika bidhaa, kuwasilisha ritani na kulipa kodi stahiki kwa wakati, kutoa taarifa za vitendo vya ukwepaji kodi pamoja na kuzingatia matakwa mengine ya sheria za kodi.

Alisema kuwa hilo litaongeza uwezo wa serikali kuendesha shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo nchini ikiwamo utekelezaji wa miradi kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, maji na uboreshaji huduma za jamii kwa ustawi wa maisha ya Watanzania.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwa mwaka huu wa fedha ambao serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 49.35, mapato ya Serikali Kuu yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 33.254.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

# REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ON THE FINANCIAL AND COMPLIANCE AUDIT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2023

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MARA REGION
00772011 - MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2023**

| | Note | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Asset** | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 62 | 2,362,705,006 | 545,173,437 |
| Receivables | 67 | 272,096,669 | 301,730,176 |
| Prepayments | 69 | 3,113,804 | 162,488,785 |
| Inventories | 70 | 603,383,052 | 178,765,113 |
| **Total Current Asset** | | **3,241,298,531** | **1,188,157,511** |
| **Non-Current Asset** | | | |
| Investment Property | 76 | 1,206,303,200 | 1,230,923,310 |
| Property, Plant and Equipment | 77 | 53,539,163,345 | 51,016,398,772 |
| Work In Progress | 82 | 1,625,082,936 | 617,082,618 |
| Investments in LGLB: LGAs To LGLB | 86 | 26,744,000 | 26,744,000 |
| **Total Non-Current Asset** | | **56,397,293,481** | **52,891,148,700** |
| **TOTAL ASSETS** | | **59,638,592,012** | **54,079,306,211** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current Liabilities** | | | |
| Payables and Accruals | 89 | 1,358,091,752 | 2,475,979,370 |
| Deferred Income | 93 | 1,333,556,705 | 181,527,492 |
| Deposits | 94 | 683,667,886 | 100,108,966 |
| **Total Current Liabilities** | | **3,375,316,343** | **2,757,615,828** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **3,375,316,343** | **2,757,615,828** |
| **Net Assets** | | **56,263,275,669** | **51,321,690,384** |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| **Capital Contributed by:** | | | |
| Other Reserves | | 26,744,000 | 26,744,000 |
| Accumulated Surpluses / (Deficits) | | 56,236,531,669 | 51,294,946,384 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | **56,263,275,669** | **51,321,690,384** |

Bosco O. Ndunguru
**Municipal Director**
Date: 24/3/2024

Hon. William P. Gumbo
**Municipal Mayor**
Date 24/3/2024

20

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MARA REGION
00772011 - MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2023**

*Classification of Expenses by Nature*

| | Note | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **REVENUE** | | | |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 0 | 300,000 |
| Levies | 18 | 895,091,328 | 669,913,074 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 1,131,291,022 | 893,114,324 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 536,879,664 | 236,262,647 |
| External Assistance | 25 | 987,592,882 | 828,579,836 |
| Other Revenue | 31 | 712,491,232 | 858,942,468 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 25,964,956,889 | 24,417,435,650 |
| **Total Revenue** | | **30,228,303,017** | **27,904,547,999** |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| **Expenses** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 19,362,874,011 | 18,648,979,469 |
| Use of Goods and Service | 35 | 3,167,438,485 | 3,675,030,791 |
| Maintenance Expenses | 36 | 323,626,940 | 1,201,098,344 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 37 | 955,751,429 | 850,154,425 |
| Depreciation of Investment Property - Carried at Cost | 38 | 57,391,110 | 56,735,690 |
| Loss on Disposal of Assets | 44 | 0 | 9,603,252,546 |
| Other Expenses | 52 | 241,737,862 | 129,674,779 |
| Social Benefits | 56 | 987,592,882 | 820,780,836 |
| **Total Expenses** | | **25,096,412,719** | **34,985,706,880** |
| **Transfer** | | | |
| Other Transfers | 60 | 190,305,012 | 173,202,734 |
| **Total Transfer** | | **190,305,012** | **173,202,734** |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | **25,286,717,731** | **35,158,909,614** |
| **Surplus / (Deficit)** | | **4,941,585,286** | **(7,254,361,616)** |

Bosco O. Ndunguru
**Municipal Director**
Date: 24/3/2024

Hon. William P. Gumbo
**Municipal Mayor**
Date 24/3/2024

21

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MARA REGION
00772011 - MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

**STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSET / EQUITY FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2023**

| | Tax Payer's Fund TZS | Accumulated Surplus/(Deficit) TZS | Other Reserve TZS | Total TZS |
|---|---|---|---|---|
| **Opening Balance as at 01 Jul 2022** | **0** | **51,294,946,384** | **26,744,000** | **51,321,690,384** |
| Surplus/ (Deficit) for the Year | 0 | 4,941,585,286 | 0 | 4,941,585,286 |
| **Closing Balance as at 30 Jun 2023** | **0** | **56,236,531,670** | **26,744,000** | **56,263,275,670** |
| **Opening Balance as at 01 Jul 2021** | **0** | **58,549,308,000** | **26,744,000** | **58,576,052,000** |
| Surplus/ (Deficit) for the Year | 0 | -7,254,361,616 | 0 | -7,254,361,616 |
| **Closing Balance as at 30 Jun 2022** | **0** | **51,294,946,384** | **26,744,000** | **51,321,690,384** |

Bosco O. Ndunguru
**Municipal Director**
Date: 24/3/2024

Hon. William P. Gumbo
**Municipal Mayor**
Date 24/3/2024

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MARA REGION
00772011 - MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

**CASHFLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2023**

| | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | |
| **RECEIPTS** | | |
| Subvention from other Government entities | 26,554,139,178 | 23,879,208,597 |
| Social Contributions (Revenue) | 536,879,664 | 236,262,647 |
| Revenue from Exchange Transactions | 0 | 300,000 |
| Other Revenue | 712,491,232 | 858,942,468 |
| Levies | 895,091,328 | 669,913,074 |
| Increase in Deposit | 583,558,920 | 0 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 1,131,291,022 | 893,114,324 |
| External Assistance | 1,008,287,372 | 828,579,836 |
| **Total Receipts** | **31,421,738,716** | **27,366,320,946** |
| **PAYMENTS** | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 19,668,352,910 | 18,653,452,509 |
| Use of Goods and Service | 3,955,634,978 | 4,082,803,386 |
| Social Benefits | 987,592,882 | 820,780,836 |
| Other Transfers | 58,845,085 | 167,050,985 |
| Other Expenses | 241,737,862 | 129,674,779 |
| Maintenance Expenses | 323,626,940 | 1,201,098,344 |
| Decrease in Deposit | 0 | 115,442,034 |
| **Total Payments** | **25,235,790,657** | **25,170,302,873** |
| **NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | 6,185,948,059 | 2,196,018,072 |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | |
| **Investing Activities** | | |
| Payment for Work in Progress | -1,625,082,936 | -487,082,618 |
| Advance Payment for Acquisition of Property Plant and Equipment | 0 | -160,415,665 |
| Acquisition of Property, Plant and Equipment | -2,619,906,944 | -1,610,943,352 |
| Acquisition of Investment Property | -32,771,000 | 0 |
| | -4,277,760,880 | -2,258,441,635 |
| Land Debts Settlements | -90,655,612 | 0 |
| **Total Investing Activities** | -4,368,416,492 | -2,258,441,635 |
| **NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | -4,368,416,492 | |
| | | -2,258,441,635 |
| Net increase/(decrease) in cash and cash equivalent | 1,817,531,569 | -62,423,563 |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | 545,173,437 | 607,597,000 |
| Cash and cash equivalent at end of period | 2,362,705,006 | 545,173,437 |

Bosco O. Ndunguru
**Municipal Director**
Date: 24/3/2024

Hon. William P. Gumbo
**Municipal Mayor**
Date 24/3/2024

23

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MARA REGION
00772011 - MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

**RECONCILIATION OF NET CASH FLOWS FROM OPERATING ACTIVITIES TO SURPLUS/(DEFICIT) FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2023**

| | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|
| **Surplus/ (Deficit) for the Period** | 4,941,585,286 | -7,254,361,616 |
| **Add/ (Less) Non Cash Item** | | |
| Depreciation of Investment Property - Carried at Cost | 57,391,110 | 56,735,690 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 955,751,429 | 850,154,425 |
| Loss on Disposal of Assets | 0 | 9,603,252,546 |
| Non-Monetary Revenue - Capital | -81,200,000 | 0 |
| Non-Monetary Revenue - Current | -460,952,434 | -359,208,545 |
| Use of Goods and Service | 323,170,277 | 206,381,758 |
| **Add/ (Less) Change in Working Capital** | | |
| Deferred Income | 1,152,029,213 | -179,018,508 |
| Inventories | -264,113,051 | -132,748,113 |
| Other Receipt | 583,558,920 | -115,442,034 |
| Payables and Accruals | -1,027,232,006 | -474,676,410 |
| Prepayments | -1,040,684 | 1,948,880 |
| Receivables | 7,000,000 | -7,000,000 |
| **Net Cash Flow from Operating Activities** | 6,185,948,059 | 2,196,018,072 |

Bosco O. Ndunguru
**Municipal Director**
Date: 24/3/2024

Hon. William P. Gumbo
**Municipal Mayor**
Date 24/3/2024

### 1.2.2 Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines

**Subject Matter: Budget formulation and execution**
I performed a compliance audit on budget formulation and execution of Musoma Municipal Council for the financial year 2022/23 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.

**Conclusion**
Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, Budget formulation and execution of Musoma Municipal Council is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

**(i) Diversion of approved development funds to finance unbudgeted recurrent activities TZS 132,594,824**
Musoma Municipal Council implemented and paid TZS 112,779,623.83 from LGAS Development account for activities for which there were no budget provisions for them during the financial year 2022/23.

I also noted that, the Council budgeted TZS 14,000,000 from development funds (own source) for operations of Council's Bricks Fabrication Project where by TZS 4,000,000 was budgeted for procurement of mould for 5 inches bricks and TZS 10,000,000 for procurement of cement. However, it was revealed that, TZS 33,815,200 were actually spent from LGA's Development Account for the operations of the said project resulting into excess expenditure by TZS 19,815,200. This is not only against the requirements of Section 27 (4) and 41 of the Budget Act, 2015 but also, negatively affect the implementation of annual approved activities.

**(ii) Under-allocation of own source revenues to development activities 478,170,126**
Musoma Municipal Council collected TZS 1,903,050,122.27 net of protected revenues collections of which TZS 761,220,048.91 which is 40% of the collected amount was supposed to be allocated for implementation of development activities including transfer to Women, Youth and People with Disability Fund (WYDF). However, only TZS 224,204,837.09 and TZS 58,845,085.76 was allocated to development activities and WYDF implying that TZS 478,170,126 was not allocated. This is against the requirements of Para 83 (iv) of the Guideline for Preparation of Government Plans and Budget for the financial year 2022/23.

Wendy W. Massoy
**Acting Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania,**
**March 2024**



## Kiteto yapewa mamilioni kwa miradi elimu

**Na Allan Isack,** KITETO

SERIKALI kuu imetoa Sh. milioni 949.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya elimu wilayani hapa Mkoa wa Manyara.

Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita Kisau, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa eneo hilo.

"Ndugu wananchi wenzangu wa Jimbo la Kiteto, nachukua fursa hii, kuwafahamisha tumepokea Sh. 949,200,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Nimezungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa na amethibitisha pesa zimetumwa na Mkurugenzi wetu wa Halmashauti ya Wilaya ya Kiteto, Hawa Hassan Abdul, amenithibitishia kupokea fedha hizo na zitatumwa kwenye maeneo husika bila kuchelewa," alisema Ole Lekaita.

Alisema fedha hizo zitatumika kwa ujenzi wa shule ya msingi mpya ya Olmugi iliyopo Kata Namelock na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu sita ya vyoo shule za msingi Orgira Kata ya Sunya.

Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu sita ya vyoo shule ya msingi Nalangitomon iliyopo Kata ya Partimbo.

Vyumba vitatu vya madarasa, matundu sita ya vyoo na madarasa na vyoo ya mfano ya awali shule ya msingi Kurash,Kata ya Lengatei.

Vilevile zitatumika kwa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu sita ya vyoo shule ya msingi Enguserosidan ya Kata ya Laiseri.

"Tutajenga vyumba vitatu vya madarasa na matundu sita ya vyoo shule za msingi Orkitikiti (Engangongare), Kata ya Lengatei," alisema.

Mbunge huyo, alisema fedha hizo, zitatumika kujenga nyumba ya walimu katika shule ya sekondari ya Ndirigish kwenye Kata ya Ndirigish.

"Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiteto, tunamshukuru sana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake wote serikalini kwa kutupatia kiasi hiki cha fedha kwa kuwa zitakwenda kuchochea shughuli za maendeleo kwa wananchi.

"Pia tunamshukuru rais wetu, kwa kuendelea kuboresha maisha yetu, wana Kiteto kwa kuendelea kutuletea miradi mikubwa ya maendeleo na kushughulikia changamoto za wananchi katika wilaya yetu," alisema Ole Lekaita.

Akizungumzia kuhusu ahadi za Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema zinaendelea kutekelezwa kwa kushirikiana wananchi wa Kiteto na wana sababu ya kutoa shukrani kwa Rais Samia.

Alitoa wito kwa watumishi na wananchi kuhakikisha miradi hiyo inalindwa na kusimamiwa vizuri na kwa ufanisi ili kulenda maendeleo na watu wapate huduma hizo kwa wakati.

# Askofu Shoo ataka mafunzo ya unyago, jando kunusuru ndoa kuvunjika nchini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Frederick Shoo ameitaka serikali, viongozi wa dini, mila na malezi kurejesha mafunzo ya jando na unyago katika jamii ili kunusuru ndoa nyingi kuvunjika nchini.

Dk. Shoo alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro na wajumbe 390 wa Idara ya Malezi ya Dayosisi hiyo.

Alisema viongozi hao wanapaswa kurudi kuwafunda vijana, kuwaandaa kuchukua majukumu ya kuwa mume na mke ili kunusuru ndoa nyingi kuvunjika.

"Pale msingi inapotetereka, hakika matokeo yake tunayaona katika kuvunjika kwa ndoa, kuharibika kwa ndoa. Maana yake ni nini? vijana wetu hawajaandaliwa, hawajalelewa katika kuchukua majukumu. Hawaelewi maana ya ndoa ni nini, hawaelewi maana ya kuishi mume na mke, wajibu wao ni kitu gani," alisema na kusisitiza kuwa:

"Tunapoona hakuna umuhimu wa kuwaandaa vizuri vijana hawa, basi matokeo yake, ndio tunayoyashuhudia sasa. Kwa hiyo mimi niseme, utumike muda wa kutosha, viongozi wa dini, viongozi wa malezi katika jamii kwa ujumla, hata wale wa kimila iwafundishe vijana wetu, tuwaandae vizuri katika kuchukua majukumu ya kuwa mume na mke."

Askofu Dk. Shoo, alifafanuwa kuwa mafunzo hayo lengo lake ni kuwafundisha vijana jukumu la kubeba wajibu wao kama mume, mke na mzazi.

"Nafikiri hilo ndilo linalohitajika kufanyika na tusifikirie tu kwamba tunaweza kufanya kwa akili zetu. Ndio kuna akili na maarifa mengi kutokana na uzoefu na taaluma, pia kuna jambo la kumcha Mungu," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho, alisema ndoa na unyumba vikitunzwa, watoto watalelewa vizuri na kutokea jamii yenye afya.

"Sasa hivi tunazungumzia tatizo la afya ya akili lakini ukiangalia msingi wake ni watu wameacha hofu ya Mungu. Msingi wake watu wameacha kutunzana, kuleana mpaka inafikia mtu anaharibikiwa, anapatwa na msongo wa mawazo. Watu wanapata mambo mazito ambayo hawana mtu wa kuwasaidia, kwa hiyo tushirikiane wote kujenga familia imara," alisema.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo akizungumzia kuhusu masuala ya talaka, wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Bungeni Jijini Dodoma alisema:

Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umesajili hati za talaka 866 mwaka 2023, ikilinganishwa na hati za talaka 447 zilizosajiliwa mwaka 2022.

Kwa mujibu wa RITA, umesajili hati za viapo vya ndoa 45, 455, ikilinganishwa na hati za viapo vya ndoa 51,011 mwaka 2022.

Awali, Katibu wa Idara ya Malezi wa Dayosisi hiyo, Mchungaji Faustina Mmari Kahwa, alisema mkutano huo mkuu wa 41 wa idara hiyo, uliketi kutoa taarifa ya kazi zilizofanywa kwa muda wa miaka minane.

Kwa mujibu wa Mchungaji Kahwa, wajumbe wa mkutano huo wanaotoka katika sharika zote 173 za Dayosisi hiyo ya Kaskazini.

# Wanaoharibu utalii kwa kukata miti waonywa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa ameonya kuwa serikali haiko tayari kuona baadhi ya watu wanaharibu uchumi wa Arusha unaotegemea utalii kwa kung'oa miti kupisha ujenzi wa makazi na kutozingatia tathimini ya athari ya uharibifu wa mazingira (EIA).

Amesema wanaoharibu mazingira kwa kukata na kung'oa miti hovyo, wanapaswa kujiandaa kisaikolojia kukabiliana na mkono wa sheria, kwa sababu Arusha inategemea wakati wote uchumi wake utalii unaotokana na kuvutia wageni kutokana na hali nzuri ya hewa na mazingira ya asili.

Mtahengerwa, alikuwa akizungumza jana na wadau mbalimbali katika Hospitali ya Jiji la Arusha iliyoko Njiro wanaopambana na uharibifu wa mazingira, ikiwamo Benki ya Kimataifa ya NCBA inayoendesha kampeni yake ya kupanda miti 1,000 jijini humo.

"Tukiiharibu hii hali ya hewa, maana yake tunaharibu uchumi wa watu wa Arusha; na sisi kwa kweli kwa jambo hilo hatuko tayari liharibike kwenye mikono yetu.

...na ndio maana tunajitahidi sana, tunaunga mkono taasisi, mashirika na asasi zote ambazo zinajihusisha na utunzaji wa mazingira ili kukuza uchumi wa taifa na Arusha kwa ujumla kupitia utalii.

"Kwetu sisi Arusha, tuna bidhaa nyingi ambazo tunauza. Bidhaa ya kwanza ni utalii. Tunao utalii wa kawaida, tuna utalii wa mikutano, na sasa hivi tumeongezewa utalii wa michezo na utalii wa hali ya hewa."

Kuhusu kampeni hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCBA Tanzania, Claver Serumaga, alisema kati ya miti 1,000 itakayopandwa kuipamba Arusha, 700 ni ya kivuli na 300 ya matunda kwa ajili ya kuboresha lishe ya wananchi.

"Tunatambua umuhimu mkubwa wa kuhifadhi rasilimali zetu asilia, kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa na kukuza maendeleo endelevu. Kwa kupanda miti, hatuimarishi tu uzuri wa mandhari yetu, bali pia tunachangia ustawi wa jamii zetu na afya ya sayari yetu kwa ujumla.

"Zaidi ya hayo, jitihada hii ya kupanda miti ni sehemu ya jitihada kubwa NCBA Group. Miradi kama hii imefanywa na NCBA nchini Kenya, ambapo wenzetu walipanda miti mwaka jana na wataendelea kufanya hivyo mwaka huu."






# Wavuvi wagomea waraka wa serikali

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

BAADHI ya wavuvi katika Mwalo wa Bwiro Wilaya ya Ukerewe mkoani hapa wamesema hawapo tayari kufuata waraka wa serikali juu ya ukomo wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria kwa madai ni kikwazo kwao kujitafutia riziki.

Juni 15, 2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya sheria ya uvuvi sura ya 279, kifungu cha 4(3) ilitoa waraka wa matumizi ya wavu kwa uvuvi wa dagaa katika ziwa hilo.

Waraka huo ulieleza kuwa serikali ina jukumu la kusimamia, kulinda na kuendeleza raslimali za uvuvi nchini, katika kusimamia uvunaji endelevu wa dagaa ziwani humo, ilipiga marufuku matumizi ya nyavu zisizokuwa na ukomo, hivyo kusababisha kuvuliwa samaki wachanga.

Waraka huo ulitaja samaki hao kuwa ni sangara na aina nyingine wasiokusudiwa na kwamba hali hiyo kuwa inasababisha uharibifu wa mazingira, mazalia ya samaki na kutishia uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

Kufuatia kifungu hicho cha sheria waraka huo uliagiza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wavuvi kutumia wavu wenye urefu usiozidi mita sitini na kina cha mita 20.

Kadhalika ulitaka umbali kati ya boya na boya usizidi sentimeta 20, ukubwa wa tundu la wavu usipungue milimita nane, uvuvi ufanyike katika umbali usiopungua mita 2,000 sawa na kilomita mbili.

Vilevile waraka huo ulitaka uvuvi huo kufanyika mchana na usiku wa mbalamwezi kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya 65(1) ya uvuvi ya mwaka 2009 na ilivyofanyiwa marekebisho na kutangazwa mwaka 2020.

Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Profesa Mohammed Sheikh alionya kuwa ukiukwaji wa waraka huo ni kinyume cha sheria kwa kuwa umelenga kulinda ikolojia ili kuwa na uvuvi endelevu wa samaki, uhifadhi wa mazingira na mazalia ya samaki ziwani humo.

Kufuatia waraka huo, wavuvi hao wameiomba serikali kuufanyia marekebisho kwa madai kuwa umeelekeza kwa wavuvi wa dagaa ambao ndio wahusika wakuu wa mazao tajwa.

"Nyavu tunazozitumia zimehalalishwa na serikali yenyewe, lakini leo hii tunabadilishiwa na kutakiwa kubadili tena na gharama tunaingia sisi," alisema mvuvi Wambura Mwita.

"Hapa kuwafungia wavuvi wa dagaa ni kuzifungia riziki na ajira zetu vijana basi watutafutie ajira nyingine kwani sisi huku ziwani hatuna mashamba," alisema mvuvi mwingine, Constantine Kulisekwa.

Akizungumza kwa njia ya simu Mwenyekiti wa Umoja wa Wavuvi Tanzania, Bakari Kadabi, alithibitisha kupokea waraka huo na kueleza kuwa ni sehemu ya matokeo ya mkutano baina yao na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kujadili kukabiliana na upungufu wa mazao ya samaki ziwani humo.

Kadaba, alisema makubaliano yalikuwa ni aidha kufunga ziwa hilo au yawekwe marekebisho, lakini ilibainika nyavu zilizopo zinatumiwa vibaya na baadhi ya wavuvi kuvua sangara wachanga.

"Nawashauri wakubaliane na waraka huu wala wasiogope kwani hiyo kanuni siyo msaafu kwamba usibadilishwe maana ikitokea haujakaa sawa tutakaa tena na wizara ili tuone namna ya kuliweka sawa," alisema Kadabi.

# Hifadhi SACCOS yakopesha wanachama mamilioni

**Na Halima Ikunji,**
TABORA

CHAMA cha akiba ya kuweka na kukopa cha watumishi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kimekopesha wanachama wake zaidi ya Sh. bilioni 150 kwa ajili ya kuboresha maisha yao.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja wa hifadhi hiyo, Ibrahim David wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika mkoani hapa.

David, alisema chama hicho cha Hifadhi SACCOS Ltd kilichopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kilianzishwa kwa lengo la kuwainua kiuchumi watumishi wa mamlaka hiyo ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema malengo mengine ni wanachama wake kujiwekea akiba hadi wanapostaafu.

"Mwanachama anaweza kukopa kuanzia Shilingi milioni 20 na kuendelea ili aweze kufanya shughuli ambazo atakuwa ameanzisha na kununua hisa na kuwa sehemu ya mmiliki wa SACCOS.

Mmoja wa wanachama wa chama hicho, Abushi Ismail, alisema amenufaika kwa kujenga nyumba bora, kusomesha watoto kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo.

Ismail, aliwashauri watumishi nchini kujiunga katika vyama kwa ajili ya kujiendeleza na kuinua hali yao ya uchumi.

# Kizazi hodari kuendelea kuwanufaisha vijana

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

VIJANA wenye umri chini ya miaka 18 katika mikoa tisa nchini wataendelea kunufaika na Mradi wa USAID Kizazi Hodari, unaotekelezwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Mshiriki anayesimamia Matokeo na Asasi zinazotekeleza mradi huo katika Kanda ya Kaskazini Mashariki, Aminiel Mongi wakati wa kikao cha tathimini ya utekelezaji wake mkoani Shinyanga.

Mongi, alisema mradi huo chini ya ufadhili wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID)

pamoja na mambo mengine umelenga kuboresha afya, ustawi na ulinzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi na vijana ili kutokomeza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

"Mradi huu unahudumia mikoa hiyo tisa, ikiwa na jumla ya halmashauri 41," alisema Mongi na kuitaja mikoa hiyo kuwa ni Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida, Dodoma, Mwanza, Geita na Mara.

Alisema lengo kuu ni kuboresha afya, ustawi na ulinzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na vijana ili kufikia malengo ya kidunia ya kupambana na UKIMWI.

Alitaja makundi yatakayofikiwa wakati wa utekelezaji wa mradi huo kuwa ni pamoja na watoto walioathirika na virusi hivyo, watoto wa wanawake walioko katika mazingira hatarishi na watoto walioathirika na matukio ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.

Mchumi Mkuu Idara ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Rashid Kitambulio, alisema serikali itaendelea kushirikiana na KKKT kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kitambulio, alishukuru USAID kwa mradi huo kuendelea kuwanufaisha waathirika hasa wa UKIMWI nchini.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Zabron Masatu, alisema mradi huo una manufaa makubwa hasa katika Sekta ya Afya na kwamba baadhi ya familia zimepatiwa ufadhili wa kadi za bima ya afya kwa ajili ya matibabu.

Mratibu wa mikoa na halmashauri wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS), aliupongeza mradi huo kuendelea kuwatambua na kuwawezesha kupata huduma zinazostahili waathirika wa UKIMWI na kushauri uwe endelevu ili kuzuia maambukizi mapya ya virusi hivyo nchini.


## NOTISI YA MNADA WA HADHARA/MARUDIO YA TANGAZO

**MANGWEMBE 2011 CO. LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **MWANGA HAKIKA BANK LTD,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tangazo hili,vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | PATRICIA ANURUPHUS MPANJU | ANURUPHUS A. MPANJU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO KUTOKA SERIKALI YA MTAA | NYAKASANGWE, WAZO,MANISPAA YA KINONDONI | 18/07/2024 NAKUENDELEA |
| 2. | RASHID ALMAS TAMBWE | RASHID ALMAS TAMBWE | AINA YA GARI NISSAN MURANO | NAMBA YA USAJILI :T 257 DXX | 19/07/2024 NAKUENDELEA |
| 3. | INCHAGHE INVESTMENT LIMITED | WINANI GEBANI WINANI | AINA YA GARI 1. KIA SPORTAGE NA 2. VOLKSWAGEN AMAROCK PICK UP | i) NAMBA YA USAJILI :T 476 DGF<br>ii) NAMBA YA USAJILI :T 672 DJQ | 19/07/2024 NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali iliyopo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hatimiliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD**
**P.O.BOX 12943, ARUSHA, TANZANIA**
**0752 632 033 AU 0628512033, Email; mangwembe@gmail.com**


Ukurasa 12

**Afrika Kusini yaunda Baraza la Mawaziri, ANC bado kinara**


Ukurasa 13

Serikali zijifunze maandamano na ghasia za kupinga kodi, ushuru


Ukurasa 14

**URAIS MAREKANI**

**Biden: Siyo kijana, bado nipo, naweza kuongoza**



# Licha ya TLP kujitutumua kuchagua M/Taifa, Ofisi ya Msajili haimtambui

• Yawaambia wameboronga huku taratibu zikikiukwa

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya mvutano wa miaka miwili, hatimaye Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), kimefanya uchaguzi wa Mwenyekiti Taifa, ambaye ni Aivan Maganza.

Hata hivyo, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, imetangaza kuwa haimtambui na uchaguzi huo haina taarifa zake.

Akichaguliwa kwa kura 35 Jumamosi iliyopita kwenye mkutano mkuu uliofanyika Dar es Salaam, anewashinda wagombea wengine Kinanzaro Mwanga na Stanley Ndamugoba waliovuna kura 10 kila mmoja, Richard Lyimo na Abuu Changaa walioambulia patupu, ni kwa mujibu wa msimamizi wa uchaguzi Dominatha Rwechungura.

Wakati Donatha, akisema hayo, ushindi wa Mwenyekiti Maganza, hautambuliwi na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa maelezo kwamba haikuarifiwa wala kualikwa na kwamba taarifa zilizopo katika ofisi hiyo ni za uchaguzi uliahirishwa.

Wakati viongozi hao wakisema wanaye kiongozi mkuu wa chama, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, anasema ofisi yake haitambui uchaguzi huo, na haina taarifa zake.

Anasema, kwa kawaida chama kinapofanya uchaguzi, ni lazima ofisi yake ipewe taarifa ya maandishi ili viongozi wake wawepo katika uchaguzi huo na kwamba haina barua wala chochote kuhusu mchakato huo.

"Taarifa iliopo ofisini ni kwamba uchaguzi umeahirishwa, sasa huo umefanyikaje wakati kuna taarifa ya kuahirishwa? Mbona ofisi haina barua ya kufanyika kwa uchaguzi huo? Anahoji Nyahoza.

Anafafanua kuwa ofisi inawasiliana na katibu mkuu wa chama kupata taarifa zote, na kwamba ilipokea barua kutoka kwa katibu mkuu ambaye ni Richard Lyimo ikielezea kuahirishwa kwa uchaguzi huo.

"Juni 29 tulikuwa tunasimamia uchaguzi wa viongozi wa Chama cha ADC kwa sababu walileta barua rasmi inayoelezea kuhusu uchaguzi wao nasi tukaenda kuusimakia, lakini huo wa TLP hatuutambui," anasema.


Aivan Maganza, Mwenyekiti TLP Taifa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**


Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, ofisi yake haitambui yaliyofanyika TLP.

**MAELEZO TLP**

Kwa mujibu wa msimamizi wa uchaguzi Dominatha Rwechungura wajumbe waliokuwapo katika uchaguzi walikuwa ni 55 Maganza akaibuka mshindi hivyo wakawa wamechagua mwenyekiti mpya wa TLP taifa.

Dominatha anasema, wamepata wakati mgumu kuandaa uchaguzi huo baada ya kuandika barua mara kwa mara kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye ni mlezi wa vyama.

"Lakini bahati nzuri tumefanikiwa kuitisha uchaguzi na sasa ninaomba wajumbe tushikamane kujenga chama chetu ambacho marehemu Mwenyekiti Augustine Mrema alikipigania kwa nguvu zake zote," anawakumbusha.

Anasema, uchaguzi huo ulifanyika nchini chini ya ulinzi wa jeshi la polisi, kwa kuwa awali uliingia dosari kwa maelezo kuwa kulikuwa na viashiria vya kufanya hujuma za kuelekea kulazimishwa kuuahirisha tena.

Katibu Mwenezi wa chama hicho, Geofray Laizar, anasema, ni wakati wa sasa wa kushikamana na kuachana na makundi kwa pamoja pasipo kuangalia dini wala kabila na kuondokana na makundi katika chama hicho.

"Baada ya kumpata mwenyekiti mpya, sasa tutaunda safu ya ushindi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa kisha kumsimamisha mgombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," anasema Laizar.

**FIGISI ZA UCHAGUZI**

Tangu kutokea kifo cha aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa, Augustine Mrema ambaye alifariki Agosti mwaka 2022, kumekuwa na danadana za kumpata mrithi wake katika nafasi hiyo.

Baada ya kifo hicho, Septemba mwaka huo, sekreterieti ya chama ilimchagua Hamad Mukadamu kuwa kaimu mwenyekiti ili baadaye ufanyike uchaguzi wa kumpata mwenyekiti taifa.

Hata hivyo, tangu wakati huo, uchaguzi umekuwa ukipangwa na kuahirishwa mara kwa mara hadi Juni 29 ulipofanyika, lakini umekataliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kutokana na sababu ambazo zimeelezwa na Nyahoza.

**INAENDELEA UK. 12**

# Afrika Kusini yaunda Baraza la Mawaziri, ANC bado kinara



Kiongozi wa DA, John Steenhuisen, akipongezana na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa. Vyama vyao vimeunda serikali ya mseto. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

RAIS Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini ameunda Baraza la Mawaziri, licha ya jina na Waziri wa Kilimo kutotolewa mapema, ila atatokana na Chama cha Democratic Alliance (DA). Wateule wengi wanatokea African National Congress (ANC).

Wizaya za Fedha na Viwanda Nishati, Usafirishaji na maeneo yamayohitaji mageuzi, mengi yamebakia ANC.

Wakati ambapo sera za umiliki ardhi hazihitaji mabadiliko ila wakulima wa Kizungu wanahitaji, nje ya maeneo ya jadi ya Wazulu na makabila makubwa kadhaa, ni eneo hilo ambalo DA ilipewa kama wizara yake muhimu ya kwanza.

Cha kushangaza ni kuwa hata wakati Rais Ramaphosa anaitoa orodha ya Baraza la Mawaziri nafasi ya Waziri wa Kilimo ilikuwa haijajazwa, hali inayoashiria

> Ila kwa nchi iliyozoea utawala wa uelekeo wa kimapinduzi, ANC ni wale watakaofufua biashara.

kuwa waziri atatoka DA lakini apatikane mtu ambaye ANC wanamkubali.

Suala la mashamba au kilimo linaweza kuwa nyeti mbele ya safari, hivyo anatakuwa waziri ambaye hatazusha matatizo na wanaharakati ANC au makundi yaliyojitoa ANC na kuunda upinzani.

Hizo ndiyo habari mpya baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa Bunge la Afrika Kusini na chama tawala cha ANC kupata chini ya asilimia 42 ya kura. Hali iliyosababisha iundwe serikali ya mseto ili kuwa na wingi wa viti bungeni.

Ramaphosa hakuchukua muda kujiweka tayari kwa hatua hiyo, ila mjadala wa ndani ya ANC kuhusu serikali ya mseto sasa umetoa hitimisho.

Ni serikali ya ANC ambako wapo wahusika wa vyama kadhaa na chama kikubwa ni DA. Hakuna ushirikiano wa kiitikadi ambako masuala ya fedha, biashara yanashikwa na DA huku ulinzi, mambo ya nchi yapo ANC.

Nyakati za Nelson Mandela akiwa rais, Inkatha Freedom Party (IFP), ilikuwa na Wizara ya Mambo ya Ndani na kukaimu urais kama Mandela na Naibu Thabo Mbeki wamesafiri. Ilijenga umoja wao kitaifa na kuondoa vurugu za makundi ya Wazulu walioona wananyanyaswa na ANC.

ANC imerudi katika mfumo wa awali kwa kushirikiana an DA, chama cha naibu wa kwanza wa Mandela, Frederick de Klerk, ambaye aliwaongoza Wazungu walio wachache kukubali utawala walao wengi. Mkataba wa ANC na IFP kuungana na DA ndiyo tangu mwanzo ulikuwa unaonekana kuunda serikali yenye tija, si ya malumbano na kuharakati kama Chama cha Jacob Zuma cha Umkhonto we Sizwe ukimaanisha mkuki wa taifa, au cha Julius Malema cha EFF kinachozungumzia kutaifisha mali za Wazungu.

Serikali thabiti kisera ni muungano wa ANC na DA, na IFP cha Wazulu wahafidhina hivyo waendana na DA, tofauti na MK au EFF. Wako waliotaka serikali ya umoja wa kizalendo lakini isingetatua lolote katika mikwamo ya uchumi na kijamii inayovuruga imani ya wapigakura kwa ANC.

Kwa vile ndiyo chama katika uundaji serikali, ANC inatakiwa itumie nafasi ya kuunda umoja wa kitaifa, kusikiliza hoja za mageuzi na kuzifanyika kazi, na siyo kubaki katika dhana kuwa hawa wa DA na IFP wamekuja tu kutafuta vyeo.

Ina maana kuwa nje ya hapa kila kitu kinawezekana, pamoja na kuwa ukiangalia hali ya kiuchumi na kisiasa nchini humo, kila aina ya mseto itakuwa na majaribu ya aina moja au nyingine kiitikadi na kisiasa, iwe ni kwa chama cha ANC chenyewe au ni kwa Rais Ramaphosa kama kiongozi.

Moja ya maeneo hayo ni kuungana na Democratic Alliance kama jumuia ya wafanyabiashara na kwa jumla wanadiplomasia wa Ulaya na Marekani wanavyotaka, huku wale wa Afrika ni kama wanaangalia tu. Ila kwa nchi iliyozoea utawala wa uelekeo wa kimapinduzi, ANC ni wale watakaofufua biashara.

Ina maana kuwa kupata muunganiko wa kiitikadi unaoiinua ANC na Afrika Kusini mbele ya macho ya dunia inabidi chama hicho kihame kutoka uasili wake na kurudi katika mwenendo wa mageuzi iliyoukataa kwa takriban miaka 25 tangu demokrasia halisi ipatikane.

Mwelekeo huo ulikuwa thabiti ukisimamiwa na Rais Mandela, aliyeacha uelekeo wa kiharakati au hata kimapinduzi kutokana na mwanga kuhusu amani na maridhiano ulioasisiwa na Askofu Desmond Tutu. Mrithi wa Mandela, Thabo Mbeki, alikwama kusititiza mwelekeo huo, itikadi ya harakati ikachukua nafasi yake, pamoja na udhaifu mwingine kwa mfano kutawala raslimali zote.

Lakini utawala wa Jacob Zuma, uliiasi ANC kutokana na mashauri ya kisheria kumepunguza kwa nguvu kura ANC, na baadhi watataka kuwepo na maridhiano na kundi la kiongozi huyo, aombwe radhi.

## Licha ya TLP kujitutumua kuchagua M/Taifa, Ofisi ya Msajili haimtambui

**INATOKA UK. 11**

Mara ya kwanza, chama kilipanga kufanya uchaguzi Januari 8 mwaka jana, lakini ukaahirishwa hadi Machi 6 2023, ukaendelea kupigwa dana dana hadi Mei mosi mwaka huo huo na ukakwama.

Baada ya hapo, ukapangwa kufanyika Desemba 28 mwaka jana, lakini haukufanyika, kisha ukapangwa kufanyika Januari 28 mwaka huu, ukaendelea kukapigwa kalenda hadi mwishoni mwa mwezi uliopita.

Awali kabla ya Juni 29,Katibu Mkuu Lyimo aliitisha mkutano na waandishi wa habari na kutangaza kuahirisha uchaguzi huo, kwa maelezo kuwa chama hakina fedha za kufanikisha uchaguzi huo.

Hata hivyo, kauli hiyo ilipingwa na upande unaomuunga mkono makamu mwenyekiti na kusema hizo ni figisi huku ukieleza kuwa wajumbe wa mkutano wa uchaguzi wanajilipia gharama zote.

Baada ya mvutano huo, upande huo wa makamu mwenyekiti ukaendelea na maandalizi ya uchaguzi huo uliofanyika Juni 29, lakini Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa I hauutambui.

Wakati makamu mwenyekiti anaandaa uchaguzi, hatimaye ukafanyika, katibu mkuu aliandika barua kwenda Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inayoelezea kuahirishwa kwa uchaguzi huo.

Kwa mujibu wa Nyahoza, barua inayoelezea kuahirishwa kwa uchaguzi huo ambayo iliandikwa na katibu mkuu ndiyo inayotambuliwa, kwa kuwa amefuata utaratibu unaotakiwa wa kutoa taarifa kwa maandishi.

# Serikali zijifunze maandamano na ghasia za kupinga kodi, ushuru

• Raia wengi ni vijana lakini wako hoi, wawatazame...

**Na Gaudensia Mngumi**

WATAALAMU wa uchumi na misaada wanakadiria kuwa Afrika imepokea zaidi ya dola trilioni moja za Marekani katika kipindi cha miaka 50 iliyopita.

Hata hivyo, bado hakuna maendeleo na nchi zinategemea misaada kutoka nje ili kujiendesha, hali inayoashiria kuwa msaada huo hauwafikii wengi na kuzidi kuongeza changamoto za kimaisha.

Aidha, kutokana na kupungua kwa misaada ya fedha kutoka nje, serikali za Afrika zikiwamo za Afrika Mashariki zimeanza kuminya kila mahali ili kupata fedha, ikiwa kuongeza na kusaka zaidi kodi.

Lakini, tahadhari ni kwamba ushuru unaweza kuwa jambo zuri hata hivyo, wakati viwango vikikithiri serikali lazima zijue kuwa zinawavunja watu migongo na huenda ikawa vigumu kupata fedha hizo.

Maandamano yanayoendelea ya kukataa kodi yanayotikisa ukanda wa Afrika Mashariki, huku ghasia na uharibifu wa mali ukionekana nchini Kenya, yanaashiria kuwa namna ya matumizi bora ya kuwaletea maendeleo kutoka kwenye kodi na ushuru wananchi wanaotozwa ni jambo ambalo huenda limeshindikana na sasa jamii inaanza kukasirika.

Uhuru wa kujieleza, haki ya kuchukua hatua, kuandamana na kupinga kutozwa ushuru, au kuadhibiwa ukidai haki yako umeanza kwa miaka mingi na sasa kizazi cha sasa cha vijana kinauongezea nguvu.

Kinachoonekana ni kukataa kutozwa ushuru bila kuwa na uwakilishi unaojali shida za raia, wananchi wanataka waone maoni yao yanatumika kwenye kupanga mipango inayoathiri mifuko yao.

Wanapenda wasikilizwe na maamuzi yanayoathiri taifa. Yaangaliwe kwanza kuliko kuwa na mipango inayoumiza watu kwa manufaa ya wachache.

Kukataa viongozi kufanya maamuzi ya kuumiza wananchi kumekuwapo tangu enzi na enzi na kuna historia zinazozungumzia Mapinduzi ya Ufaransa ambayo yanaelezwa kuwa mfalme na familia yake walikuwa wanakula na kusaza wakati Wafaransa hawana hata maji ya kunywa.

Mapinduzi ya Ufaransa yaliyoanza mwaka 1789 na kudumu hadi 1794, yanaelezwa kuwa Mfalme Louis XVI alihitaji pesa zaidi, lakini alishindwa kuongeza kodi zaidi.

Katika changamoto za ugumu wa maisha huko Ufaransa mfalme na Malkia Marie Antoinette, waliuawa 1793, na watu wakimtuhumu malkia kuwa wakati wananchi wanalalamikia kukosa mkate yeye anasema wapewe keki.

Yote hayo yalimaanisha kuwa uongozi haujui uchungu wanaopata walipa kodi na ugumu wa maisha wanayopitia. Si jambo jema kujisahau kama kiongozi kama ilivyotokea kwenye kasri la mfalme wa Ufaransa miaka hiyo.



Waandamanaji mitaani

Kinachoonekana sasa ni kwanza mataifa ya Afrika yajitafakari kwa kuangalia kanuni za ushuru na kodi, je, wananchi wanaweza kuzilipa? Ni nani hasa alipe na yupi asikatwe kodi? Kulipa kodi ni lazima lakini kunafanywa kwa haki na matumizi yake yakoje? Umma unaridhika na matumizi ya kodi hizo? Ni kwanini kuna malalamiko?

Mathalani, masoko mengi Tanzania yanalalamikiwa kuwa wafanyabiashara wanatozwa ushuru kila siku kuanzia Shilingi 500 hadi maelfu lakini sokoni hakuna vyoo, hata kama vipo ni duni na vibovu, maji ya kunywa na miundombinu ya masoko ni chakavu. Mfano Soko la Mabibo Dar es Salaam, halifikiki nyakati za mvua.

Magari kwenye vituo vya mabasi yanalalamikia kutozwa ushuru kila siku lakini stendi hazina huduma bora kama vyoo, maji ya kunywa wala unafuu wa huduma. Zina mashimo na wahusika hawajali.

Kadhalika kwenye minada ya mifugo ushuru unachukuliwa kila siku tena mara kwa mara lakini hakuna maendeleo, pengine hakuna hata choo, huduma ya chakula , maji ya kunywa na maeneo bora ya kuosha na kulaza au kuhudumia mifugo yote haya yanaelekeza wanaokusanya ushuru na kodi kutafakari njia zao.

Viongozi watambue kuwa kanuni za kuchukua kodi zinapaswa kuzingatia uwezo wa walipa kodi, lakini pia kodi hiyo inakubalika kwa sababu mfumo wa kodi wenye haki ni lazima jamii na raia waone matunda ya kodi zao na siyo kuona wachache wakineemeka na wengine wakiwa fukara licha ya kulipa kodi na ushuru.

Hata hivyo, suala la migomo ya kodi lisichukuliwe kwa wepesi kwani maandamano ya kimkakati yanayoleta ghasia, uharibifu wa mali hata kuchoma bunge na kubeba majeneza na vitisho ni hatari kwa uwekezaji na shughuli za kiuchumi.

Hatari hizo za kisiasa zinaweka mazingira magumu kibiashara na uwekezaji na kukimbiza wawekezaji wa kigeni.

Kinachoonekana kinaweza kuchukuliwa kuwa ni cha nchi moja lakini ukweli ni kwamba picha ya kutisha inasaambaa Afrika nzima na kuongeza uwezekano wa bara hili kuogopwa na wawekezaji.

Ni hatari zinazotishia wawekezaji, mashirika na serikali kwa sababu matukio kama hayo yataathiri watu wengi na mipango ya kiuchumi inayotarajiwa na hatua zilizofikiwa.

Kwa maneno rahisi, hatari ya migomo ya kodi, maandamano na uharibifu wa mali yanatishia hatima za kisiasa na kuongeza uwezekano kwamba biashara zinaweza kuharibiwa kwa sababu ya kukosekana kwa utulivu.

Migogoro na machafuko, mabadiliko ya fikra za vijana, sera za kitaifa au mahusiano kati ya nchi, sheria za biashara au kanuni za uwezekaji na masuala ya kulalamikia kodi ni mambo yanayotishia hatima ya uwanja mzima wa uwekezaji na biashara.

> “Kinachoonekana kinaweza kuchukuliwa kuwa ni cha nchi moja lakini ukweli ni kwamba picha ya kutisha inasambaa Afrika nzima na kuongeza uwezekano wa bara hili kuogopwa na wawekezaji.

**CHAKUJIFUNZA**

Ni vyema serikali ziwe na busara wakati wa kupanga namna ya kupata kodi. Sera za ushuru lazima ziwe wazi na zinazokubalika na kueleweka kwa wananchi.

Uwazi unaamanisha kuwa kutoza ushuru kwenye vyakula na kutoa msamaha wa kodi kwa magari mapya kutoka kiwandani huko ughaibuni ni jambo linaloweza kuonyesha kuwa serikali inayofanya hivyo haiwajali wananchi wake.

Serikali lazima itoe maeleza ya kutosha kwa wananchi kuhusu uhalali wa kutoza kodi na wanasiasa na uongozi wa umma waonyeshe kwa mfano kutumia kodi kwa kuleta maendeleo ya taifa na siyo kuendeleza ubadhirifu katika matumizi ya pesa ambazo wananchi wanataka zibadilishe maisha yao.

Serikali zikumbuke kuwa kundi kubwa ya raia ni vijana na wana nguvu na kuna haja kuwasaidia wawe na maisha bora ili kuwa na utulivu wa kisiasa na kijamii na kwa ujumla kuwe na uongozi bora ili kuwe na amani.

Mataifa yanahitaji kuwa na umakini kwenye ushuru na uongozi bora kwenye masuala ya matumizi ya fedha. Kadhalika kuangalia na kufanya tafiti za mara kwa mara vipi kodi zinazotozwa zinawaumizaje wananchi?


Wafanyakazi na wafanyabiashara wanalalamikia kodi ya ongezeko la thamani VAT au kodi ya mshahara PAYE serikali ziangalie na kuchambua mwelekeo wa kodi hizo na athari kwa wahusika kuepusha maandamano na kususa kufanyabiashara.

JUKWAA LA VIONGOZI

URAIS MAREKANI

# Trump: Nitamalizana na Putin 'fasta' Biden: Japo siyo kijana, bado nipo

**Na Mwandishi Wetu**




Wagombea urais Marekani 2024; Donald Trump na Joe Biden katika mdahalo wa CNN huko Atlanta, Georgia. **PICHA: VOA**

RAIS John Biden wa Marekani baada ya kuchuana na mpinzani wake, Donald Trump, kwenye mdahalo wa urais anasema bado yuko ngangari katika mbio za kuingia White House.

White House ndilo jina la Ikulu ya Marekani, ambayo Joseph Biden, anatafuta kurudi tena kuendelea kuhudumia wananchi katika kura ya Novemba 4 mwaka huu.

Anawaambia wafuasi wake kuwa bado yuko katika kinyang'anyiro tena akizungumza katika mkutano wa kampeni unaofanyika katika jimbo muhimu la North Carolina mwishoni mwa wiki.

Rais Biden alionekana mchangamfu akiwa North Carolina tofauti na alivyokuwa wakati wa mdahalo wa televisheni uliomkutanisha na hasimu wake Donald Trump, inasema DW.

Tambo hizo zinajiri baada ya kukabiliana na Donald Trump katika mdahalo wa kwanza wa uchaguzi wa rais wa 2024 nchini Marekani na kwamba katika hotuba yake ya dakika 18, kwa wanachama wa Democrat na wafuasi wake rais huyo alikuwa mchangamfu kuliko usiku uliotangulia wakati wa mdahalo huo wa televisheni.

Katika mdahalo wa kwanza wa uchaguzi wa rais wa msimu wa 2024, anasikika akitoa majibu kwa sauti inayokwaruza na wakati mwingine kupotea katika kutoa ufafanuzi wa kile anachoulizwa.

Katika Jimbo la North Carolina, rais huyo wa Marekani anakiri namna vyombo vya habari vilizungumzia alivyofanya katika mdahalo huo.

Anawaambia Waamerika kuwa yeye si kijana tena na akakiri kuwa kwa sasa hafanyi vyema katika midahalo kama alivyokuwa huko nyuma. Hata hivyo, anasisitiza kuwa anajua jinsi ya kuchapa kazi na hilo halijamshinda inaongeza DW.

Matokeo mabaya ya Biden katika mdahalo wa Alhamisi usiku wiki iliyopita yaliwafanya baadhi watu katika chama chake cha Democratic kuhoji kama anapaswa kubadilishwa na tiketi hiyo kupewa mtu mwingine.

Hata hivyo mchakato huo hauwezekani kwa urahisi isipokuwa kama Biden ataamua kujiondoa na kumpisha kijana ambaye ataperusha bendera ya chama hicho.

Katika mdahalo wa Atlanta wiki iliyopita ambao uliendeshwa na kituo cha televisheni cha CNN, Trump anasema Marekani "ni taifa lililoshindwa kabisa." Inaripoti Sauti ya Amerika VOA

Anaongeza:" Biden amefanya kazi mbaya. Mfumuko wa bei unaiua nchi yetu. Kwa hakika anatuua sisi." Inaripoti VOA

> "Biden anaeleza kuwa wakati Trump alipokuwa rais, aliwatenganisha watoto na mama zao, na kuwaweka kwenye vyumba vidogo, kuhakikisha kuwa wametengwa na familia zao.

Akizungumza kwenye kampeni, Biden anasema amebadili uchumi wa maskini ambao aliurithi kutoka kwa Trump.

Kadhalika, katika mdahalo wa Atlanta, Biden anaeleza kuwa ana mengi ya kufanywa kuhusu uchumi na utawala wake "unafanya kazi kubwa ya kupunguza bei bidhaa za vyakula, na hicho ndicho watakachokifanikisha." Inaongeza VOA.

Katika mdahalo, mgombea wa Republican Trump anasema Biden ameshindwa kuwalinda Wamarekani kutoka kwa wahamiaji haramu, ambao wanachukua nafasi za kazi. Trump: "Anaongeza kuwa Marekani ina mpaka ambao ni hatari sana kuliko sehemu nyingine yoyote duniani, ikifikiriwa ni sehemu hatari sana kuliko popote katika dunia na aliifungua, na hawa wauaji wanakuja katika nchi yetu, na wanawabaka na kuwaua wanawake."

Kwa upande Biden anapozungumza kwenye mdahalo, akiwakumbusha wapigakura kuhusu utawala wa Trump ulivyozitenga familia kwa sera yake ya wahamiaji.

Biden anaeleza kuwa wakati Trump alipokuwa rais, aliwatenganisha watoto na mama zao, na kuwaweka kwenye vyumba vidogo, kuhakikisha kuwa wametengwa na familia zao."

Kuhusu vita vya Ukraine, Trump anasema Rais wa Russia Vladimir Putin, asingeivamia Ukraine kama yeye angekuwa rais wa Marekani.

Trump anahidi kuwa kama rais mteule, atahakikisha kuwa vita hivyo vinasuluhishwa kati ya Putin na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy, tena kabla ya kuapishwa Januari 20, atakuwa amesuluhisha vita hivyo na mambo yatatulia.

Lakini Biden anamgeukia Trump akisema kutokuwa na uungaji mkono na washirika wa Marekani kumeimarisha Russia na kutishia kuwa na vita vikubwa huko Ulaya na ndicho kinachoonekana leo.

Biden anasema: "Putin anaitaka Ukraine yote. Ndicho anachokitaka. Halafu unadhani atasimama hapo tu? Unadhani ataacha, kama akiichukua Ukraine, nini kitatokea kwa Poland na Belarus?" inasema VOA.

Mdahalo wa wiki iliyopita ulikuwa wa mapema wa urais katika historia ya Marekani, japo si Trump wala Biden aliyeteuliwa rasmi kutwaa nafasi ya ugombea wa chama. Wanasiasa hao wana siku zaidi ya 70 za kuwashawishi wapigakura kuwachagua kabla ya mdahalo mwingine utakaofanyika Septemba.

## TRUMP HASHTAKIWI

Wakati huo huo, Mahakama ya Juu ya Marekani juzi Jumatatu, imetoa maamuzi kuwa rais wa zamani Donald Trump, ana kinga kwa matendo yote rasmi aliyofanya ya kujaribu kubadili kuchaguliwa mwaka 2020, lakini hana kinga kwa matendo yasiyo rasmi.

Mahakama hiyo kwa uamuzi huo imeziachia mahakama za chini kufanya maamuzi ni kesi zipi ambazo Trump anaweza kufunguliwa mashtaka, kwa mujibu wa VOA.

Uamuzi huo wa majaji sita dhidi ya watatu kwenye siku ya mwisho ya muhula wa sasa wa mahakama unamhakikishia Trump kuwa hatashtakiwa katika kesi kabla ya uchaguzi wa Novemba 5 ambapo yeye ni mgombea mteule wa chama cha Republican, akitarajiwa kukabiliana tena na Rais Joe Biden, wa Democrat aliyemshinda katika uchaguzi wa 2020.

Trump amekanusha kufanya kosa lolote linalohusishwa na matokeo ya uchaguzi wa 2020 lakini kwa muda mrefu amekuwa akidai kulikuwa na matatizo katika kupiga kura na kuzihesabu kulikomfanya ashindwe kupata muhula mwingine wa miaka minne ndani ya White House.

Kama akishindwa katika uchaguzi wa Novemba, huenda mara tu akakabiliwa na kesi inayohusishwa na uchaguzi wa 2020, lakini kama akishinda, anaweza kumuelekeza mwanasheria mkuu, mwendesha mashtaka mkuu wa nchi, kuachana na kesi hiyo.

Mahakama Kuu ilikuwa ya kwanza kufanya maamuzi iwapo rais zamani huenda akashtakiwa kwa kesi ya uhalifu kwa vitendo vyake alivyofanya wakati akiwa madarakani, au kama ana kinga ya kumzuia kushtakiwa.

Msingi wa sheria za Marekani unaelezea wazi kwamba hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, kuwa kila mtu ana uhuru sawa lakini kila mmoja anaweza kushtakiwa kwa kuvunja sheria.

Trump alidai kuwa ana kinga ya kiutendaji, akisema kwamba kumshtaki kwa kujaribu kubadili kushindwa kwake miaka minne iliyopita, alikuwa akichukua hatua kama rais akijaribu kuimarisha uadilifu katika matokeo, akisisitiza kwamba alishindwa kwasababu ya wizi na matatizo mengine katika uchaguzi. **VOA**





## ‘Wanasiasa msiogope kuchangia makanisa, misikiti’

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati mkoani Singida, limewataka wanasisa kuacha kuogopa kuchangia maendeleo kwenye misikiti na kanisani kwa kuhofia kuhusishwa na kampeni za kisiasa.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kati Singida, Dk. Cyprian Hilinti, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa harambee ya pili ya kanisa hilo ya kukusanya kiasi cha Sh. milioni 700 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya ujenzi wa seminari Kiomboi, Kititimo Complex, kufungua duka la dawa, kukarabati Shule ya Sekondari Ihanja na Hospitali ya Iambi.

“Wanasiasa msiwe mnaogopa kutoa msikitini na kanisani kusema nitaonekana nafanya kampeni hizo ni fedha zako hujachukua za mtu na kudhani utaitwa kwenye kamati za ndani,” alisema.

Askofu Dk.Hilinti, alizitaka kamati za ndani za kanisa kuacha tabia ya kuwaita wanasiasa wanaotoa au kuchangia kwenye miradi ya taasisi za dini ili kuondoa dhana potofu miongoni mwa jamii.

Akizungumza katika harambee hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Mkumbo, alisema kanisa lina kazi kuu tatu za kujenga afya ya kiroho, ya mwili ambazo zinajengwa hospitali na ya akili ambayo ndio nafasi ya elimu.

Alisema ni hatari kuhubiri injili kwenye tumbo lenye njaa na kichwa chenye njaa ya akili.

“Ukikuta waumini hawana elimu ndio wanapeperushwa kwenda kufanya mambo mengi ya ajabu, hivyo elimu ni muhimu sana kwasababu inahitajika hata katika kutafakari neno la Mungu,” alisema Prof. Mkumbo ambaye alikuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk.Mwigulu Nchemba.

Alisema wanasiasa na viongozi wa dini wanafanana kwa kuwa wote wanatoa neno, wao wanahutubia siasa na wenzao wanahubiri.

“Sifa inayotuunganisha dini na siasa wote ni watu wa kuahidi na hilo tunalimudu, siasa tunaahidi kuishusha mbingu kuja duniani halafu kanisa linaahidi kuchukua dunia kuipeleka mbinguni,” alisema na kuongeza:

“Wanasiasa tunatoa ahadi tunasema mkinichagua mimi mtafurahi sana nitawaletea maji, barabara na nitaongeza kipato, sasa ukiongeza kipato si utanunua gari utafurahi, sasa dini wanahubiri ili muishi kwa furaha shikeni neno, lakini yote ni furaha ama furaha ya hapa duniani au ya mbingu.”

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema serikali itaendelea kushirikiana na taasisi za dini kwa kuwa inatambua kazi nzuri zinazofanya na kuleta maendeleo.

# TASUPA yajitosa kukabili uagizaji mafuta nje

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wasindikaji Mafuta ya Kula ya Alizeti Tanzani (TASUPA) kimeandaa mikakati kukabili uhaba wa mafuta ya kula nchini na kuiondolea mzigo serikali wa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kuagiza nje bidhaa hiyo.

Mwenyekiti wa TASUPA, Ringo Iringo, alitangaza mpango huo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati hiyo ya kukabili uhaba wa mafuta ya kula nchini.

Iringo, alisema mikakati hiyo ni kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Wizara ya Kilimo na halmashauri nchini kuandaa na kuhamasisha uwekezaji wa mashamba makubwa na ya kati ya kibiashara kuzalisha alizeti.

“Tunategemea pia mipango ya serikali kuwekeza na kuimarisha na kukamilika kwa wakati miundombinu ya umwagiliaji ili baadhi itumike katika mashamba makubwa ya uwekezaji ya uzalishaji wa alizeti, ” alisema.

Alisema wataanza kuhamasisha kilimo cha alizeti kwa misimu miwili katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Mbeya, Kagera, Kigoma, Morogoro,Tanga, Katavi, Ruvuma, Lindi na Mtwara.

“ Tunategemea kuanza mwaka huu 2024 wakati wa mvua za vuli,” alisema.

Iringo, alisema kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wenye mapenzi na sekta ndogo ya alizeti, watahamasisha na kuwajengea uwezo wakulima wadogo zaidi ya milioni mbili nchini kulima alizeti kitaalamu na kisasa.

“Sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali itaanzisha utafiti wa kupatikana kwa mbegu zenye mafuta mengi na matumizi yake kwa wakulima na kwa kushirikiana na TABEDO, tutahamasisha ufugaji nyuki pembeni mwa mashamba ya alizeti ili kuwezesha uchavushaji wa alizeti, kuongeza mavuno na kipato kwa wakulima,” alisema.

Alisema wakulima wengi nchini wamekata tamaa baada ya kukosa soko la alizeti kutokana na mafuta kutoka nje kuwa mengi, hivyo kusua sua katika kilimo kwa kupunguza uzalishaji.

“Nchi haitakuwa na upungufu mkubwa wa mafuta ya kula kwani tunaanza kulima alizeti mpya kwa wingi pindi msimu wa vuli utakapoanza mapema Septemba mwaka huu,” alisisitiza Iringo.

Kadhalika, alisema uwekezaji katika mashamba makubwa na madogo ya kibiashara unaendelea mikoa ya kimkakati chini ya mpango wa serikali.

Alisema katika miaka mitatu ijayo Tanzania inatarajia kuzalisha zaidi ya tani milioni tano za alizeti peke yake, kusindika mita za ujazo 900,000 kwa mwaka na kulisha hitaji la nchi na ziada ya kuuza nchi za nje.



Waziri wa Afya, Dk. Ummy Mwalimu (kushoto), akijadiliana jambo na Mwenyekiti wa Hospitali ya macho ya Charitable Eye Centre, Anver Rajpal, wakati wa maadhimisho ya miaka mitatu ya hospitali hiyo, Temeke, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wa (pili kushoto) ni Rais wa Jumuiya ya Khoja Shia Ithnaashari, Alhadji Mohammedrazza Dewji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa dini wafundwa kwa migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa dini wametakiwa kujiepusha na migogoro ili kuisaidia serikali kulinda amani na utulivu nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Msajili wa Jumuiya ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Thomas Sanira kwenye ibada ya kuwasimika maaskofu watano wa dayosisi, iliyofanyika Kanisa la Free Anglican Church of Tanzania Mtakatifu Simoni Petro Usharika wa Ilazo Dodoma.

Sanira, alisema migogoro mingi kwenye taasisi za dini inatokana na kugombea madaraka na mali na kuikosesha serikali kupata misaada.

Alisema serikali inategemea mchango wa taasisi hizo za dini kuiombea nchi amani, utulivu na viongozi wake waliopo madarakani, hivyo ni wajibu wa taasisi hizo kuepuka migogoro.

“Hivyo niwaombe maaskofu wa madhehebu ya dini kujiepusha na migogoro ambayo haina tija bali waifanye kazi waliyoitiwa na Mungu kukemea vitendo viovu,” alisema.

Aliwataka viongozi dini kushirikiana na serikali kukemea ukiukaji wa maadili, kuiga mila na desturi za nje ambazo zimekuwa zikichangia vijana wengi ambao ni tegemeo la Taifa kujiingiza katika vitendo visivyo faa.

Vilevile, aliwataka waumini kuepuka kuwa chanzo cha migogoro kwa viongozi wao kwenye nyumba za ibada.

Awali akihubiri kwenye ibada hiyo Mchungaji Ruth Chimalusotola, aliitaka serikali kukemea na kuwachukulia hatua viongozi wanaoshindwa kuwajibika kwenye nafasi zao.

“Bado kuna tabia ya kulindana kwa baadhi ya viongozi kwa wale ambao wapo chini yenu mnashindwa kuwaondoa hata kama wameharibu na kushindwa kufikia malengo yanayotakiwa kwenye maeneo yao na kwa jamii pia, ” alisema.



# Polisi waagizwa kumsaka kijana kwa kumkashifu Rais Samia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapa limeagizwa kumsaka na kumtia mbaroni kijana mmoja, mkazi wa Kijiji cha Ntokela Wilaya ya Rungwe kwa tuhuma za kumkashifu Rais Samia Suluhu Hassan mitandaoni.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera wakati akizungumza na wandishi wa habari kwa njia ya mtandao akiwa nchini China.

Homera alisema kuwa jeshi hilo linatakiwa kumsaka na kumkamata mtuhumiwa huyo ambaye picha zinamuonyesha mitandaoni akimtukana Rais Samia.

Mtuhumiwa huyo ambaye jina lake halijafahamika, alionekana akiwa ameshika picha ya Rais Samia huku akitamka maneno ya kashfa ikiwemo kumtuhumu kuwa ameshindwa kulilinda taifa.

Mtuhumiwa huyo baada ya kutamka maneno hayo, alionekana akiimwagilia picha hiyo mafuta yanayodhaniwa kuwa ya taa kisha kuichoma moto jambo ambalo limetafsiriwa kuwa ni kashfa dhidi ya kiongozi huyo mkuu wa nchi.

"Hii video inakuhusu wewe mwenyewe (Rais Samia) na siyo mtu mwingine, umeshindwa kutetea taifa lako najitambulisha kwamba nipo Mkoa wa Mbeya, Kijiji cha Ntokela wilayani Rungwe," alisikika mtuhumiwa huyo akisema.

Homera, alisema kitendo alichokifanya mtuhumiwa huyo ni kinyume na maadili na tamaduni za watu wa Mkoa wa Mbeya, na kuliagiza jeshi hilo atafutwe na ndani ya saa 24 awe amekamatwa ili achukuliwe hatua kali za kisheria.

Alisema mtuhumiwa huyo ameonekana kutokuwa na nia njema na viongozi wa nchi hivyo ni lazima achukuliwe hatua ili iwe fundisho kwa wananchi wengine wenye mawazo kama hayo.

"Kwanza sisi kama serikali tunalaani vikali tukio la kijana huyo la kuwakashifu viongozi wetu wa kitaifa na huu sio utamaduni wa wananchi wa Mbeya, kwa hiyo naagiza Kamanda wa Polisi amsake popote alipo ili achukuliwe hatua," alisema Homera.

Aliwasisitiza wakazi wa Mbeya kuwaacha viongozi wao wafanye kazi ya kuwaletea maendeleo na wasigeuke kuwa kikwazo cha kuwakatisha tamaa.

Akizungumza kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Katibu wa Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile, alisema kinalaani vikali tukio lililofanywa na mtuhumiwa huyo kwa maelezo kuwa linakiuka taratibu za nchi.

Uhagile alisema Rais Samia alitoa msimamo wa taifa kuhusu masuala mbalimbali yanayokwenda kinyume na sheria za nchi, hivyo mtuhumiwa huyo hajalitetea taifa ni kumkosea heshima.

Alisisitiza kuwa Rais Samia alishatoa msimamo wa Taifa kuhusu vitendo vinavyokiuka utamaduni wa Kitanzania na hivyo lazima kila mwananchi avipinge na kuagiza kila mmoja lazima azingatie mila na desturi za nchini.

Alisema kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu ya Jumuiya za CCM, ya Wazazi ndiyo iliyokabidhiwa mamlaka ya kusimamia maadili ya taifa na ndiyo iliyoagizwa kupinga vitendo hivyo.



Baadhi ya wakulima wakiianika kahawa kwenye vichanja vya kisasa katika Kijiji cha Halungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe hivi karibuni, baada ya kupata mafunzo kutoka kwa wadau wa zao hilo ili kuzuia kushuka ubora na kuathiri soko. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafanyakazi kiwanda cha chai wagoma

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYAKAZI wa Kiwanda cha Chai cha Kampuni ya DL Group kilichopo Mtaa wa Kibena Kata ya Ramadhani mkoani hapa wamegoma kushinikiza kulipwa mishahara ya miezi minne.

NIPASHE lilifika kiwandani hapo jana na kushuhudia wafanyakazi hao wakiwa wamekusanyika nje ya lango wakidai hawajalipwa mishahara yao hiyo na stahiki nyingine.

Walidai kutolipwa mishahara hiyo kwa kipindi hicho, kumesababisha maisha yao kuwa magumu na kushindwa kumudu gharama za maisha yao na familia.

Walidai kuwa hali hiyo ambayo pia imechangia kushindwa kuwapeleka watoto shule, pia imechangia mitaani kukosa uaminifu wa kukopesheka.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Chesco Mligo, alisema wanachoomba ni kulipwa mishahara ili waweze kuendesha maisha yao ambayo yamekuwa magumu kutokana na uwepo wa tatizo hilo kwa muda mrefu sasa.

"Tunataka mishahara yote ya miezi minne, tumetumika na kudanganywa vya kutosha lakini sasa uvumilivu umeishia hapa," alisema Chesco Mligo.

Legnand Joseph, alisema wamefanya kazi kwa muda mrefu katika mazingira magumu bila ya kupata stahiki zao.

"Inasikitisha, tunafamilia, ndugu wanaotutegemea na maisha ni magumu, mishahara miezi minne si mchezo," alisema Joseph.

Alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati ili walipwe mishahara yao na stahiki nyingine.

Levina Mgunda alisema mashine katika kiwanda hicho ni mbovu na kulazimika kufanya kazi katika mazingira magumu kutokana na miundombinu ya kizamani.

Meneja wa Kiwanda hicho, Gerad Ngenzi alisema hawezi kuzungumza lolote kwa kuwa si msemaji.

Hivi karibuni Mkurugenzi wa DL Group, David Lingat alikutana na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka kujua ni lini kampuni hiyo italipa madeni ya wafanyakazi hao.

Lingat alimueleza mkuu wa mkoa kuwa kuna changamoto ya biashara ya chai na si katika kampuni hiyo pekee bali katika sekta ya chai.

Alisema wanaweka mikakati ya kutafuta suluhisho kwa kushirikiana na serikali ili waweze kutatua changamoto.

# Wadau washauriwa malezi ya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa maendeleo ya awali ya watoto mkoani hapa wameshauriwa kuwashirikisha viongozi wa dini na wa mila katika utekelezaji wa afua za Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Elizabeth Nyema alitoa ushauri huo kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa huo kwenye kikao cha mapitio ya robo ya pili ya utekelezaji wa Programu PJT-MMMAM.

Dk. Nyema alisema bado mchango wa viongozi wa dini unahitajika katika kuibadilisha jamii kutoka kwenye mfumo wa malezi wa mazoea kwa watoto na kwenda kwenye malezi yaliyo sahihi yatakayoimarisha makuzi sahihi kwa watoto.

Alisema afua tano zinazosimamiwa kwenye programu ni muhimu zikaeleweka vyema kwa viongozi wa dini na mila ili wazisisitize kwa jamii kwakuwa wana watu wengi wanaowasikiliza na kuwaamini kwenye maeneo yao.

Alisema kila mdau anatakiwa kujipima namna ambavyo ameshiriki kutekeleza afua hizo na kuweka bayana matatizo aliyokutana nayo ili zitafutiwe ufumbuzi.

"Tukiwa kwenye vikao hivi vya mapitio kila mdau aguswe na kueleza amefanya nini tangu kuzinduliwa kwa programu hii, tujione tumefika wapi na kama kuna vikwazo tuviainishe na tutoke na jawabu la nini kifuatie," alisema Elizabeth kwenye kikao hicho kilichowakutanisha wadau kutoka halmashauri zote saba za mkoa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Shalom Development Organization (SHADO) ambalo linafanya kazi ya uchechemuzi wa shughuli zinazotekelezwa chini ya PJT-MMMAM mkoani Mbeya, Padri Furaha Ntasamaye, alisema ni muhimu wadau wakashirikiana kuhakikisha watoto wana ukuaji timilifu.

Padri Ntasamaye, alisema iwapo wazazi na walezi wataendelea kutoa lawama za mapungufu ya kitabia waliyonayo watoto wa sasa,wakumbuke kuna sehemu walifanya uzembe kusimamia malezi.

Ofisa kutoka Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto, Lovenes Mtemi, alisema kuna athari za kudumu iwapo mtoto anafanyiwa ukatili kwenye umri mdogo, hivyo ni muhimu wadau wakasimama kwenye malezi yasiyomweka mtoto kwenye mazingira ya kujiona ananyanyaswa.



## Jamii yatakiwa kuwajengea uwezo watoto kujilinda

**Na Mwandishi Wetu**

JAMII imetakiwa kutilia mkazo ushiriki wa watoto katika michezo ili kuwajengea uwezo na ujuzi wa stadi za maisha kukabiliana na udhalilishaji wa kijinsia.

Wito huo ulitolewa na wadau katika kongamano la mashindano ya riadha kwa wanafunzi wa shule za Zanzibar yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

TAMWA Zanzibar, waliandaa mashindano hayo kwa kushirikiana na Idara ya Michezo, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Taasisi ya Maendeleo ya Mashirikiano ya Ujerumani (GIZ) na Kituo cha Mijadala kwa Vijana (CYD) kwa lengo la kuhamasisha usawa wa kijinsia katika michezo.

Akizungumzia juhudi za kuimarisha usawa wa kijinsia na kuhamasisha michezo kwa maendeleo, Dk. Mzuri Issa, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, alisisitiza umuhimu wa kuendeleza na kuhamasisha michezo kwa wote ili kukuza ushiriki wa jinsi zote katika michezo.

"Tuwe mifano mizuri ya kuwa na heshima katika jamii, kwasababu sisi tuna nafasi ya kupata mawaidha sehemu mbalimbali ya stadi za maisha. Hivyo tuna kila sababu ya kuendeleza kuimarisha na kuhamasisha michezo kwa wote," alisema Dk. Mzuri.

Wanu Ali Makame, Meneja Idara ya Mitaala na Vifaa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, alisema katika kutilia mkazo umuhimu wa michezo kwa maendeleo, wizara imeweka somo maalum linaloelezea masuala ya michezo.

"Tuna somo maalum linaloelezea masuala ya michezo kwa maendeleo. Tunaweza tukacheza na tukasoma kwa salama na amani bila kuathiri hulka na tabia ya mtu yeyote yule aliyetuzunguka." alisema.

Hija Ramadhan wa GIZ, alisema jitihada za kutengeneza usawa wa kijinsia ni pamoja na kuhakikisha waadau wanashirikiana kuwalinda watoto na wanawake dhidi ya ukatili.

Katika hafla hiyo hayo wanafunzi walipata fursa ya kushiriki mbio fupi na washindi kuzawadiwa zawadi mbalimbali ikiwemo medali na madaftari.

Mashindano hayo yamewaweka pamoja wanafunzi wa shule za Unguja, wanamichezo, walimu wa michezo na wadau wa masuala ya usawa wa kijinsia yakiambatana na kaulimbiu "Wakati ni sasa! Wekeza katika elimu na michezo kwa watoto wote", ikiwa ni hatua muhimu kuhakikisha michezo inatumika kama chombo cha kuleta maendeleo na usawa katika jamii.

# Usafiri wa anga kuzidi kukuza uchumi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Muhammed amesema usafiri wa anga utaongeza kasi ya kukua kwa uchumi visiwani hapa.

Dk. Muhammed aliyasema hayo jana wakati akizindua safari za ndege ya Jambojet katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume visiwani hapa.

Alisema usafiri wa ndege hiyo, pia unazidi kuwaweka pamoja ndugu wa familia moja kati ya Mombasa Kenya na Zanzibar kwa sababu historia, mila na tamaduni zinazofanana.

Alisema usafiri huo utazidisha kasi ya maendeleo kiuchumi na biashara baina ya Zanzibar na Mombasa kwa kuwa kuna wajasiriamali wengi.

Dk. Khalid, alisema pia watalii walioko Mombasa wangependa kutoka katika jiji hilo kufika Zanzibar, hivyo huduma hiyo ya usafiri itawasaidia.

"Wizara yetu inahusika na masuala ya miundombinu, lakini tunafanya kazi kwa karibu na wizara ya utalii na bahari nzuri uwanja huo wa Abeid Amani Karume umeshazindua safari za ndege nyingi na sasa kuna mashirika karibu 80 yanayokuja hapa na yanasaidia kuleta watalii," alisema.

Alisema kwa sasa Zanzibar ina watalii wastani wa 620,000 na kwa mwaka ujao inatarajia kupokea watalii 800,000 na kutaka huduma za uwanja ziendani na kasi ya ukuaji.

Alisema jengo la tatu la abiria katika uwanja huo lina uwezo wa kupokea abiria milioni 1.6 kwa mwaka, lakini mwaka 2023 walikuwa karibu milioni mbili hivyo uwezo wa uwanja umezidiwa.

Waziri huyo alisema serikali imeona ipo haja ya kuongeza uwezo kwa kujenga upya jengo la abiria la kwanza ili liwe na uwezo wa kuchukua abiria milioni tatu kwa mwaka.

Alisema ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Disemba mwaka huu ujenzi huo na kujenga jingine la abiria la nne ili uwanaj huo kuwa na uwezo wa kuchukua abiria kati ya milioni sita kwa mwaka.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema kuwa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya usafiri wa anga ili kukuza zaidi uchumi visiwani hapa hasa utalii.

Balozi wa Kenya nchini, Isaac Njenga, alisema kuwa Jambojet inakwenda kuunganisha usafiri wa maeneo muhimu kibiashara, kiutalii na kiutamaduni miongoni mwa Tanzania na Kenya.

"Kwa niaba ya serikali ya Kenya ninayofuraha leo kuwa sehemu ya uzinduzi wa safari hii mpya. Hatua hii ni muhimu kurahisisha huduma ya usafiri wa anga kati ya Zanzibar na Mombasa kwani kila mtu ataweza kusafiri kwa haraka na bei rahisi," alisema Balozi Njenga.

Gavana wa Mombasa, Abdulswamad Shariff Nassir, ambaye alisafiri kwa Jambojet kwa ajili ya kushuhudiauzinduzi huo, alisema kuwa mji wa Mombasa ni sehemu muhimu katika utalii wa Kenya kama Zanzibar kwa Tanzania.

Nassir, alisema kuanza safari za ndege hiyo, kutaongeza fursa zaidi za utalii na biashara kati ya miji hiyo ya pwani ya Bahari ya Hindi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jambojet, Karanja Ndegwa, alisema zaidi wanakwenda kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya usafiri wa anga kwa kufanya safari za uhakika na nafuu kutoka Zanzibar na Mombasa.




Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme Zanzibar, Haji Mohammed Haji (katikati), akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa uuzaji umeme kwa kutumia huduma ya simu na benki, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kasi ujenzi Makunduchi yamkwaza kigogo

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema kasi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Makunduchi inarudisha nyuma dhamira ya Rais Dk. Hussein Mwinyi kuondoa changamoto ya elimu kwa wanafuzi wa mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Abdulla aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema Serikali imeilipa Kampuni ya Fuchs Construction Limited shilingi bilioni 4.08 kuharakisha kukamilisha ujenzi huo, lakini bado unasuasua na kupelekea wanafunzi kuendelea kufuata elimu mbali na makaazi yao.

Abdulla alionya kuwa kama kampuni hiyo itashindwa kumaliza ujenzi wa shule hiyo na nyinginezo kwa wakati, itakuwa imejinyima fursa ya kufanya kazi Zanzibar.

Alisema lengo la Serikali ni kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi na kuwekeza zaidi katika sekta ya elimu.

Makamu huyo wa pili wa rais pia alifanya ziara katika Shule ya Sekondari ya Hasnuu Makame kukagua ukarabati wa jengo la bweni la wasichana baada ya kuungua moto na kusababisha hasara kwa wanafunzi.

Aliwataka walimu na wanafunzi kuendelea kulitunza na kufanya usafi ndani na nje ili jengo hilo lidumu na kutumika kwa muda mrefu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Abdulla aliuagiza uongozi wa Wizara ya Elimu kujengea uzio wa shule hiyo ili kuimarisha ulinzi na usalama kwa wanafunzi na mali zao.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali , Ali Abdulghulam Hussein, alisema wamejipanga kuhakikisha kila shule inaipatia vifaa vya kisasa vya ili kuboresha mfumo wa elimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**SCOLASTICA AGUSTINO KASHAMAKULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2120-0015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KATUMA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014 na cheti cha chuo chenye usajili namba **MBY/DPLM/16/10234** kilichotolewa na **CHUO CHA TIA MBEYA** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MBE/MBE/RH/434179/2019**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**JOSEPH THOMAS LUBAVA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA **KADI YA TREKTA** YENYE USAJILI **T687 DWJ** ILIYOPOTEA , YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/KIL/9436/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GODFREY RANGYA MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 623 EDP.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/132288/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MAULID JUMA MTETA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **KINGLION** yenye usajili namba **MC 162 AHH,** CHASSIS NAMBA: **LTBPK8B67E2K05762** na ENGINE NAMBA: **KL 157FMI 14J05762.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **HAN/RB/217**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MANGAZA MOHAMED ABALLAH** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye usajili namba **T 896 EFC,** CHASSIS NAMBA; **ANH100132634** na ENGINE NAMBA: **2AZB173822.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/131936/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**HERRY MARO MBOYA** anatangaza kupotea kwa hati ya nyumba yenye no. **174 BLOCK 'W'** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/NJO/NJO/2602/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 11950 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AUGUSTINO ISACK MMASSI DECEASED OF TAMBUKA RELI/AMANI STREET, DODOMA CITY COUNCIL**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MWAJABU SHABANI MBARUKU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16 day of 7 ...................... 2024
Dated at Dodoma this 6 Day of 6................2024

RESIDENT MAGISTRATE

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Vyama vya siasa Ufaransa kuungana

**PARIS,** Ufaransa

VYAMA vya siasa vya upinzani nchini Ufaransa viko katika mkakati wa kuungana kwa lengo la kukizuia kuwa na wingi wa viti bungeni chama cha siasa kali za mrengo wa kulia cha National Rally (RN) kinachoongozwa na Marine Le Pen.

Hatua ya vyama hivyo inajiri baada ya chama cha RN kupata mafanikio ya kihistoria kwa kushinda duru ya kwanza ya uchaguzi wa Bunge.

Matokeo rasmi yaliyotangazwa jana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ufaransa yalikipa ushindi chama cha RN cha Le Pen asilimia 33 ya kura, kikifuatiwa na kundi la vyama vya mrengo wa kushoto lililojipatia asilimia 28.

**Pia matokeo hayo yalionyesha kuwa vyama vya siasa za wastani ikiwemo cha Rais Emmanuel Macron cha Muungano wa pamoja kilipata asilimia 20 tu ya kura.**

Pia matokeo hayo yalionyesha kuwa vyama vya siasa za wastani ikiwemo cha Rais Emmanuel Macron cha Muungano wa pamoja kilipata asilimia 20 tu ya kura.

Ililezwa kuwa matokeo hayo yamekuwa pigo kubwa kwa Macron ambaye alilazimika mwezi Juni kuitisha uchaguzi wa mapema baada ya chama chake kupata matokeo mabaya katika uchaguzi wa Bunge la Ulaya.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa uwezo wa kuunda serikali kwa chama hicho cha RN, itategemea na mafanikio ya vyama vya siasa za wastani na vile vya mrengo wa kushoto katika azma yao ya kuungana katika duru ya pili ya uchaguzi na hivyo kumzuwia Le Pen kuwa na wingi wa viti bungeni.

Wagombea wa chama cha RN ambacho kimejengeka katika sera ya kuwapiga vita wahamiaji na kuipinga taasisi ya Umoja wa Ulaya (EU), walipata matokeo mazuri katika mamia ya maeneo ya bunge kote nchini Ufaransa.

Vile vile, ilielezwa kuwa vongozi wa vyama vya mrengo wa kushoto wa 'New Popular Front' na kile cha siasa za wastani cha Rais Emmanuel Macron, walidhihirisha ishara ya muungano wao kwa kusema wagombea wao katika baadhi ya wilaya wangejiondoa.

Walisema hatua hiyo itafikiwa ili kutoa nafasi nzuri zaidi kwa mgombea pinzani kupata ushindi dhidi ya mgombea wa RN katika duru ya pili ya uchaguzi huo wa Bunge, itakayofanyika Julai 7, mwaka huu.

Kadhalika, haikuwa wazi kuwa makubaliano hayo yatatekelezwa na chama cha siasa kali za mrengo wa kushoto cha 'La France Insoumise' (LFI) kinachoongozwa na Jean-Luc Melenchon, ambacho pia ni mojawapo ya chama kikuu katika muungano huo wa 'New Popular Front'.

Waziri wa Fedha Bruno Le Maire, ambaye ni mshirika wa chama tawala cha Macron, alitoa wito kwa wapiga kura kutochagua mgombea wa LFI, akisema chama hicho ni hatari kwa taifa.

Inaelezwa kuwa Tofauti za kisera, mivutano na maslahi ya kisiasa vilivyopo baina ya vyama hivyo inahatarisha azma yao ya kuungana na kumzuia Le Pen kuwa na udhibiti wa Bunge.

Mchambuzi wa taasisi inayoshughulikia na kura za maoni ya Ipsos Mathieu Gallard, alisema duru ya kwanza ya uchaguzi imeacha uwezekano kwa vyama vya siasa kugombea jumla ya viti 306 kati ya 577 vinavyowaniwa katika bunge, akisisitiza kuwa duru ya pili imegubikwa na hali ya kutokuwa na uhakika wa chama gani kitaibuka na ushindi. **DW**



Wafaransa wakipiga kura katika duru ya kwanza ya uchaguzi wa Bunge, juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Idadi ya waandamanaji waliofariki Kenya yafikia 39

**NAIROBI,** Kenya

TUME ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu nchini Kenya (KNCHR) imesema idadi ya waliofariki dunia imefikia 39 huku 361 wakijeruhiwa tangu kuanza kwa maandamano ya kupinga mswada wa Fedha 2024 kote nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na tume hiyo jana, uchunguzi wa maiti kwa wengi wa waathiriwa bado haujafanywa, huku ikibainisha kuwa kumekuwa na taarifa za watu kutekwa nyara na kukamatwa kiholela.

"Kuna visa 32 vya upotevu wa kulazimishwa au kupotea bila kukusudia na 627 vya kukamatwa kwa waandamanaji," ilisema taarifa ya KNCHR.

Pia ilielezwa kuwa baadhi ya watu wanasemekana kuwa mafichoni kutokana na vitisho dhidi ya maisha yao na watu wasiojulikana.

Katika ripoti ya tume hiyo imeendelea kushutumu utumiaji wa nguvu kipita kiasi dhidi ya waandamanaji na wengineo kama wafanyakazi wa afya, waandishi wa habari na kwenye maeneo salama kama vile makanisa na vituo vya dharura vya matibabu.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa serikali haijathibitisha idadi hiyo lakini Rais William Ruto Juni 30, mwaka huu, wakati wa kikao na wanahabari, alisema kufikia wakati huo waliofariki walikuwa 19.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa maofisa wa polisi walitekeleza majukumu yao kwa njia huru wakati wa maandamano hayo.

Vile vile, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani tayari maandamano yameanza katika maeneo kama vile Mombasa licha ya Rais Ruto kutangaza Jumatano iliyopita kwamba hatatia saini muswada huo unaopendekeza ongezeko la ushuru kwenye bidhaa kuwa sheria. **BBC**

# Wapalestina waendelea kutangatanga



**GAZA,** Palestina

WANANCHI nchini Palestina wameendelea kutangatanga baada ya Israel kutoa amri ya kuwahamisha katika baadhi ya maeneo ya Khan Younis na sehemu jirani, ikielezwa kuwa huenda agizo hilo linaashiria Israel inapanga kuushambulia tena mji huo wa Kusini mwa Gaza.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres, Stephane Dujarric alisema hatua hiyo inaonyesha kwa mara nyingine kwamba hakuna mahali salama huko katika Ukanda wa Gaza, akisisitiza kwamba juhudi zaidi zinahitajika kulinda wananchi hao.

Mkazi ambaye anaishi katika eneo ambako watu watahamishwa, Ahmad Najjar, aliiambia AFP kwamba woga na wasiwasi mkubwa umewakumba watu baada ya amri ya kuhama, na kwamba aliona idadi kubwa ya wakazi wakihama.

Ililezwa kuwa amri hiyo ya kuwahamisha watu inajiri wakati kukiwa na taarifa kwamba Israel ilimuachia huru mkurugenzi wa hospitali kuu ya Gaza Mohammed Selmia juzi kama sehemu ya kuachiliwa kwa Wapalestina kadhaa ambao walirejea Gaza kwa ajili ya kupewa matibabu.

Pia ilielezwa kuwa Selmia, amekuwa akizuiliwa tangu mwezi Novemba, 2023 na kwamba alikuwa akiongoza hospitali ya Shifa huko Gaza ambayo ilivamiwa na wanajeshi wa Israel mwezi huo, huku wakidai kuwa wanamgambo wa Hamas walikuwa wakitumia kituo hicho kama kamandi yao. **VOA**

HABARI MICHEZO

# AZAM: HAKUNA OFA YOYOTE YA SIMBA KUMTAKA FEI TOTO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam, imesema haijapokea ofa yoyote kutoka Simba ya kumtaka kiungo mshambuliaji wao, Feisal Salum Fei Toto', kama inavyodaiwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya juzi jioni kuibuka kwa kasi tetesi za mchezaji huyo kutakiwa na Simba, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Thabit Zacharia maarufu Zaka Zakazi, alisema kwa sas hakuna klabu yoyote nchini inayoweza kumng'oa Fei Toto kwenye kikosi hicho kutokana na kiasi kikubwa walichokiweka kwenye kuvunja mkataba ambapo hata Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini imeshindwa.

**"Hatujapokea ofa yoyote kutoka Simba ya kumtaka Feisal, habari za tetesi kama hizi huwa ni nyingi na ndiyo raha ya soka, lazima ziwapo ili kunogesha, na mashabiki kuchangamka kwa sababu hakuna soka linalochezwa uwanjani kipindi hiki," alisema Zaka Zakazi.**

Alibainisha kuwa uvumi huo umetokea baada ya kudaiwa kuwa amefuta utambulisho wake kwenye moja ya mtandao wake wa kijamii anaoutumia.

Zaka alisema hali hiyo ililеta sintofahamu kiasi cha kumchanganya mpaka mchezaji mwenyewe kwani tangu afute utambulisho wa Klabu ya Yanga, hakuwahi tena kuandika ni mchezaji wa timu gani, zaidi ya Timu ya Taifa, Taifa Stars.

"Watu wanahusisha hili kwa kile kilichoelezwa kuwa amefuta utambulisho wake kwenye moja kati ya mtandao wake wa kijamii kuwa ni mchezaji wa Azam. Ukweli ni kwamba hakuwahi kuandika kama ni mchezaji wa Azam, ila aliandika muda mfupi tu baada ya uvumi huu kutokea, kusema kweli hata mchezaji mwenyewe alishangaa kwa sababu, katika mtandao wa kijamii alijitaja tu kuwa mchezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, sasa sijui imekuwaje mpaka ikasemekana kuwa amefuta," alisema.

Alisema uvumi huo ulimchanganya Fei Toto ambaye sasa ili kupunguza maneno akalazimika kuingia kwenye mtandao wake na kuandika ni mchezaji wa Azam FC.

"Ni kwambie tu hakuna klabu yoyote hapa Tanzania kwa sasa inaweza kumchukua Fei Toto kutokana na kipengele tulichokiweka katika mkataba kama akitaka kuondoka, Mamelodi Sundowns wenyewe walikuja hapa kumtaka, lakini bei ikawashinda, hivyo mashabiki wa Azam wawe na imani tu, Feisal tunaye," alisema Mkuu huyo wa Idara ya Habari na Mawasiliano.

KAKOSA!...




Mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, akikosa mkwaju wa penalti katika muda wa nyongeza (extra time)kwenye mechi ya Euro 2024 hatua ya 16-bora dhidi ya Slovenia, iliyopigwa Uwanja wa Deutsche Bank Park, Frankfurt nchini Ujerumani juzi. Hata hivyo, Ronaldo alisawazisha makosa yake baada ya kufunga penalti nyingine timu hizo zilipomalia dakika 120 kwa suluhu na kuingia kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti na Ureno kushinda 3-0.
**PICHA: MTANDAO**

# *Coastal Union yasaka mbadala wa Lawi*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union hivi sasa ipo kwenye mazungumzo na beki wa kati, Issah Yakubu wa Klabu ya Stade Malien ya Mali kwa ajili ya kuziba pengo la Lameck Lawi ambaye hatokuwa kwenye kikosi hicho tena msimu ujao.

Taarifa zinaeleza kuwa Coastal, imeanza mazungumzo hayo licha ya kwamba wana upinzani mkali kutoka Klabu ya Rayon Sports na APR za Rwanda ambazo nazo zinawania saini ya mchezaji huyo.

Kwa sasa Coastal imekuwa ikihaha kusaka wachezaji wa kimataifa kutokana na msimu ujao itacheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, huku beki wao kisiki, Lawi akitangazwa kuwa mchezaji wa Simba, ingawa wenyewe wamepinga, ikidaiwa wanataka kumuuza nje ya nchi.

"Tupo makini sana na usajili, hatutaki kusajili wachezaji wa kigeni ambao watakuja kukaa benchi, tunakata mgeni wa kuja kucheza, kwa hiyo tuko kwenye mazungumzo na beki huyo, ni mzuri na anagombaniwa pia na Klabu za Rayon na APR, lakini sisi inaonekana tunaweza kushinda kwa sababu anaonekana kuvutiwa na soka la Tanzania na nchi yenyewe kwa ujumla, anaambiwa na wachezaji wenzake wa Afrika Magharibi wanaocheza huku kuwa Bongo ni sehemu sahihi kwake hata kuonekana na klabu zingine kubwa," alisema mtoa taarifa huyo.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri, amekiri kuwa kwa sasa wapo katika harakati za kufanya usajili na itafanya hivyo kwa wachezaji wa kigeni tu na ni wale waliowahi kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho tu.

"Tunataka kusajili wachezaji wasiopungua watano kwenye kikosi chetu kuelekea msimu ujao, ambapo sifa ya kwanza ni lazima awe na uzoefu wa mechi za kimataifa, kwa maana ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, ina maana ni lazima atoke kwenye klabu ambazo zimeshiriki michuano hiyo, kwani tunataka huo uzoefu tuulete kwenye klabu yetu ya Coastal, hilo ndilo ambalo linatufanya mpaka sasa tuchelewe hata kuwatangaza kwani mchakato wa kuwapata wachezaji wa aina hiyo ni mkubwa na migumu," alisema.

## Wanawake soka Iringa kuchaguana mwisho wa mwezi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Iringa (IRWFA), kimepanga kufanya uchaguzi mkuu wake ifikapo Julai 30, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Chama Cha Soka Mkoa wa Iringa (IRFA), Amos Makono, aliliambia gazeti hili maandalizi ya uchaguzi huo yanaendelea vema na fomu kwa wadau wanaotaka kugombea zitatolewa kuanzia leo hadi Julai 8, mwaka huu, katika ofisi za chama hicho.

Makono alitaja nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo ni Mwenyekiti, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TWFA na wajumbe wawili wa Kamati ya Utendaji ya IRWFA.

Naye Katibu Mkuu wa IRFA, Adinani Cholobi, alisema jana anawaomba wadau kujitokeza kuchukua fomu ili kupata viongozi watakaosimamia soka la wanawake katika mkoa wa Iringa.

"Tunahitaji viongozi ambao watajitolea kuendeleza Soka la wanawake, tunaamini watasaidia kuleta Mapinduzi," alisema Cholobi.

## Aussems apewa mwaka Singida BS

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Singida Black Stars, umemtambulisha rasmi Kocha wao Mkuu, Patrick Aussems, ambaye atainoa timu hiyo msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Jonathan Kasano, alisema kocha huyo amesaini mkataba wa mwaka mmoja huku wakiendelea na mipango mingine.

"Utambulisho huu ni miongoni mwa malengo yetu ya miaka mitatu tuliyojiwekea kuhakikisha tunakuwa na benchi bora la ufundi ambalo litaleta ushindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao kwani tunaamini huyu ni kocha mwenye uwezo mkubwa," alisema Kasano.

Alisema baada ya kupata fursa ya kushiriki mashindano ya CECAFA kwa sasa timu yao ipo jijini Dar es Salaam ikijiandaa na michuano hiyo itakayofanyika visiwani Zanzibar pamoja na Dar es Salaam.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GORDON ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL inamtaka Anthony Gordon, 23, lakini Newcastle United inasisitiza kuwa winga huyo wa England hatauzwa. ***(Telegraph)***

### DE LIGT MIAKA MITANO

KLABU ya Manchester United, imempa beki wa Uholanzi, Matthijs de Ligt, 24, mkataba wa miaka mitano wakati wakiendelea na mazungumzo ya uhamisho na Bayern Munich. ***(De Telegraaf)***

### BRANTHWAITE NAYE ANUKIA

MANCHESTER United itachukua hatua ya kumsajili Jarrad Branthwaite, 22, iwapo Everton itapunguza bei ya nyota huyo, lakini 'The Toffees' hawana shinikizo la kifedha kumuuza mlinzi huyo. ***(Sky Sports)***

### ZAHA KUREJEA EPL

MSHAMBULIAJI wa Galatasaray, Wilfried Zaha, 31, ana nia ya kurejea Ligi Kuu England, huku West Ham, Wolves na klabu ya zamani ya Crystal Palace wakimtaka mchezaji huyo wa Ivory Coast. ***(Star)***

### ALMIRON AAWINDWA SAUDIA

KLABU moja ya Saudia inafanya mazungumzo na Newcastle United kuhusu mkataba wa kumnunua mshambuliaji wao, Miguel Almiron, 30. ***(Sky Sports)***

### RAYA SAFI ARSENAL

ARSENAL imeanzisha chaguo la kumsajili kipa wa Hispania, David Raya, 28, kutoka Brentford kwa mkataba wa kudumu baada ya muda wa mkopo. ***(Mail)***

### RABIOT AGOMBEWA

LIVERPOOL na AC Milan zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 29, baada ya kumalizika kwa mkataba wa mchezaji huyo pale Juventus. ***(Calciomercato)***

### SAMBA HUYOOO SEVILLA

SEVILLA iko tayari kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na Ubelgiji, Albert Sambi Lokonga, 24, kwa mkopo wa msimu mzima. ***(Teamtalk)***

### ATAKIWA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton iko tayari kutoa dau la pauni milioni 20 kumnunua kiungo wa kati wa Celtic na Denmark, Matt O'Riley, 23. ***(Talksport)***

### STEPHENSON NA EVERTON

KLABU za Brighton, Brentford, Everton na Southampton zinavutiwa na kiungo wa kati wa Millwall, Josh Stephenson, 18. ***(Football Insider)***

### ISAAK KUBAKISHWA

KLABU ya Newcastle United imejitolea kusalia na mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, 24, huku kukiwa na taarifa zinazomhusisha mchezaji huyo na uwezekano wa kuhamia Arsenal au Chelsea. ***(Football London)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AMWAGA CHOZI URENO, UFARANSA ZIKIFUZU

**BERLIN,** Ujerumani

Ni baada ya kukosa penalti dakika za nyongeza, kabla ya kufuta makosa yake kwa...

CRISTIANO Ronaldo alibubujikwa machozi baada ya penalti yake kuokolewa katika muda wa ziada, lakini Ureno bado walifuzu robo fainali ya Euro 2024 kutokana na ushindi wa penalti 3-0 dhidi ya Slovenia.

**Nahodha huyo nyota wa Ureno alishuhudia penalti yake ikiokolewa na kipa wa Atletico Madrid, Jan Oblak na kufarijiwa na wachezaji wenzake, huku mashabiki wakiimba jina lake uwanjani.**

Lakini alipata ahueni na kufunga penalti ya kwanza kwa nchi yake kwenye mikwaju ya penalti - ambapo kipa Diogo Costa aliokoa mikwaju yote - kabla ya Bernardo Silva wa Manchester City kufunga mkwaju wa ushindi.

Ronaldo alipambana akitafuta bao lake la kwanza kwenye Euro 2024.

Kabla ya penalti yake kuelekezwa kwenye lango, alipoteza nafasi nzuri katika dakika ya mwisho ya muda wa kawaida, akipiga shuti lililoelekea moja kwa moja hadi kwa Oblak, baada ya krosi zake nyingi kupaa juu ya kichwa chake katika dakika 120 za mchezo huo mkali.

Wakati huo huo, bao la kujifunga la Jan Vertonghen liliipeleka Ufaransa katika robo fainali ya Euro 2024 kwa kuishinda Ubelgiji.

Mchezo ambao haukuwa na ubora na msisimko kwa muda wote ulionekana kupangiwa muda wa ziada, lakini shuti lililopigwa na mchezaji wa akiba Randal Kolo Muani lilimgonga Vertonghen na kuingia kimyani zikiwa zimesalia dakika tano kuhitimisha ushindi huo kwenye Uwanja wa Dusseldorf Arena.

Ufaransa walikuwa wamepoteza nafasi nyingi kabla ya hapo kwani kwa mara nyingine tena kupungua makali kwa timu yao kuliwaangusha, na hata nahodha Kylian Mbappe aliweka juhudi lakini alipiga nje mashuti mengi.

HABARI MICHEZO

# DE BRUYNE: BADO SIJAAMUA KUSTAAFU




**DUSSELDORF,** Ujerumani

KEVIN de Bruyne amesema ni mapema mno kufikiria mustakabali wake katika soka la kimataifa baada ya Ubelgiji kufungwa bao 1-0 na Ufaransa katika hatua ya 16-bora kwenye Euro 2024 Jumatatu.

Bao la kujifunga la Jan Vertonghen la dakika ya 85 lilikuwa tofauti kati ya mataifa hayo mawili kwenye Uwanja wa Arena Dusseldorf huku De Bruyne akiona nafasi nyingine ya kushinda michuano mikubwa na Ubelgiji ikitoweka.

De Bruyne mwenye umri wa miaka 33, alikuwa sehemu ya kikosi cha 'Mashetani Wekundu' kilichomaliza nafasi ya tatu kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, lakini wameshindwa kufuzu nusu fainali kwenye michuano mikubwa tangu wakati huo.

"Ni mapema mno kujibu," alisema De Bruyne akiwaambia waandishi wa habari alipoulizwa ikiwa kushindwa na Ufaransa kunaweza kumalizia soka lake la kimataifa.

"Ngoja nishughulikie hili. Umekuwa msimu mrefu sana. Ninahitaji kupumzisha mwili wangu. Nitafanya uamuzi wangu baada ya majira ya joto."

De Bruyne, ambaye alianza kuichezea Ubelgiji kwa mara ya kwanza 2010 na ameichezea nchi yake zaidi ya mara 100, bado ni sehemu muhimu ya mipango ya kocha Domenico Tedesco kabla ya Kombe la Dunia nchini Marekani, Mexico na Canada mwaka 2026.

"Anajua jinsi alivyo muhimu," alisema Tedesco kuhusu maoni ya kiungo huyo wa Manchester City kwenye mkutano na wanahabari.

"Hahitaji maoni yangu kuhusu hilo kwa sababu anajua. Mara tu baada ya mchezo, ni vigumu kumuuliza Kevin maswali ya aina hii."

# Lionel Messi arejea mazoezini Argentina



**HOUSTON,** Marekani

LIONEL Messi alirejea mazoezini na Argentina Jumatatu wakijiandaa kumenyana na Ecuador katika robo fainali ya Copa America mjini Houston wiki hii.

Messi hakuwa amefanya mazoezi tangu apate jeraha la paja wakati timu yake iliposhinda bao 1-0 dhidi ya Chile Juni 25, mwaka huu.

Alikaa nje ya ushindi wa 2-0 wa Argentina dhidi ya Peru Jumamosi.

Shirikisho la Soka la Argentina lilisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alifanya mazoezi na wenzake.

Messi alishindwa kufunga katika hatua ya makundi kwa mara ya kwanza kwenye michuano ya mwaka huu, mfululizo wa mabao ambayo pia yameisha kwa Cristiano Ronaldo wakati wa michuano ya Ulaya mwaka huu.

# Chelsea yachukua straika Barca

**LONDON,** England

CHELSEA imetangaza kumsajili mshambuliaji Marc Guiu kutoka Barcelona.

'The Blues' walianzisha kipengele cha kutoa pauni milioni tano katika mkataba wa Guiu wa Barca wiki iliyopita na sasa amekamilisha uhamisho wake wa kwenda Stamford Bridge.

Taarifa ya klabu ilisema: "Chelsea inafuraha kutangaza kumsajili mshambuliaji Marc Guiu kutoka FC Barcelona.

"Mhispania huyo amekubali mkataba wa miaka mitano na The Blues, ambao unajumuisha chaguo la mwaka mmoja zaidi, na ataungana na wachezaji wenzake wapya kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya."

Guiu aliiambia TV ya Chelsea: "Ni furaha kubwa kusajiliwa Chelsea na nilitatizika kulala mbele ya safari ya hapa kwa sababu nilikuwa na furaha sana. Tangu nilipokuwa mdogo, ilikuwa ndoto yangu kucheza Ligi Kuu England.

"Sasa nina nafasi ya kuja hapa Chelsea na nitafanya bidii yangu yote kuwa na mafanikio kwa klabu."

Guiu mwenye umri wa miaka 18, alifunga mabao mawili katika mechi saba za wakubwa akiwa na Barcelona msimu uliopita na pia aliwaniwa na Bayern Munich.

Barca walishindwa kumshawishi Guiu kubaki baada ya kifungu chake cha kuruhusiwa kuondoka kutekelezwa na Chelsea.

Hivyo, Guiu anakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na Chelsea msimu huu wa majira ya joto, baada ya kununuliwa kwa Omari Kellyman kutoka Aston Villa na Tosin Adarabioyo, ambaye amejiunga kwa uhamisho huru kutoka Fulham.

Chelsea hivi karibuni itatangaza usajili wao wa nne msimu ujao, huku kiungo wa Leicester City, Kiernan Dewsbury-Hall akikaribia kukamilisha uhamisho wa kwenda Stamford Bridge.



## HABARI MICHEZO

## Yanga yamletea...

INATOKA UKURASA 24

nzima, kuna waliokuwa wananiuliza hiyo siku ndiyo tunaanza, halafu tunakwenda kwenye matukio ya kijamii, hapana, hiyo ni siku ya kilele pale Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya hapo siku hizo mbili tatu tutawatangazia siku ya uzinduzi wa jezi na ratiba zingine," alisema Kamwe.

## Simba: Mukwala, Mulate ni ufunguzi

INATOKA UKURASA 24

bao 14, akiongozwa na mshindi wa kiatu cha dhahabu msimu uliomalizika, Stephen Amankona wa Berekum Chelsea FC aliyemaliza na mabao 19.

Straika huyo anatajwa kwenda kuchukua nafasi ya Pa Omari Jobe, ambaye taarifa zinasema atatolewa kwa mkopo kutokana na kushindwa kuonyesha makali yake baada ya kusajiliwa katikati ya msimu uliomalizika.

Kwa upande wa Mutale, anakumbukwa kwa kuwachachafya mabeki wa Simba, hasa Shomari Kapombe, katika mechi ya tamasha la Simba Day Agosti 6, mwaka jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikishinda mabao 2-0, lakini pia aliwafanya anavyotaka katika mchezo wa raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika, Septemba 16, mwaka jana nchini Zambia, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2.

Mutale alikuwa mwiba kwa mara nyingine katika mechi ya marudiano, Oktoba Mosi, mwaka jana, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, zikitoka sare ya bao 1-1, Simba ikitinga hatua ya makundi kwa mabao mengi ya ugenini. Mchezaji huyo amepachika mabao manane kwenye Ligi Kuu ya Soka nchini Zambia msimu uliomalizika.

Baada ya kuachana na nahodha wao, John Bocco ambaye ameondoka na rekodi nzuri za ufungaji kwenye klabu hiyo, na tetesi za kutaka kuachana na Pa Jobe, Mukwala anaonekana kuja kushika usukani kwenye safu ya ushambuliaji ya timu hiyo akisaidiana na Freddy Michael raia wa Ivory Coast.

# IDDI AZZAN AFUNGUKA KUHUSU CHAMA YANGA

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Iddi Azzan, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kutohuzunika kwa sababu ya kuondoka kwa kiungo mshambuliaji wao, Clatous Chama, ambaye ametangazwa kujiunga na watani zao, Yanga.

Chama ameondoka Simba baada ya kumaliza mkataba wake Juni 30, mwaka huu, kutokana na klabu hiyo kushindwa kumpa kiasi cha fedha alichohitaji ili kubakia klabuni hapo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Azzan alisema Chama si mchezaji wa kwanza mkubwa kuihama klabu hiyo na kwa sasa mpira ni Biashara, hivyo wachezaji wana uhuru wa kufanya uamuzi wapi watacheza kwa msimu husika.

**Azzan alisema anaamini Simba itapata mchezaji mwingine mwenye kiwango bora zaidi ya Mzambia huyo na viongozi waliamua kuachana naye kwa kuzingatia maslahi ya klabu na si vinginevyo.**

"Chama alikuwapo Simba na kuitumikia kwa kipindi kirefu tu, akanunuliwa Morocco, akarudi tena Simba, lakini sasa ameondoka, tuwaamini viongozi wetu kwa maamuzi yao, tuamini watatuletea nyota wakali zaidi na wataisaidia timu kufanya vema," alisema Mbunge huyo wa zamani wa Jimbo la Kinondoni (CCM), Dar es Salaam.

Aliongeza kuwa mazoea ya wachezaji kucheza na 'kuzeekea' katika klabu moja kwa sasa hayapo na hii inatoka na makubalinao yanayofikiwa baada ya kumaliza mkataba wa awali.

"Tutapata mchezaji mzuri kuliko Chama, tukubaliane na uamuzi uliofanywa na viongozi wetu, inawezekana wameona kwa sasa hatumhitaji au hawawezi kumpa kile alichokihitaji, na Yanga wamempa kwa sababu wanaamini atawafaa, " aliongeza Azzan, ambaye ni mwanachama wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao.

Simba inaendelea kufanya usajili wake wa wachezaji wapya wa ndani na nje na wameanza kuwasili jijini tayari kwa maandalizi ya kuelekea Ismailia, Misri kuweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano.

Hata hivyo, Simba bado haijatangaza rasmi mrithi wa Kocha Abdelhak Benchikha, ambaye aliachana na timu hiyo zikiwa zimebakia mechi chache za msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## MTU KATI...



Mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, akiwa amewekwa mtu kati wakati akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Ufaransa; Aurelien Tchouameni (kushoto) na William Saliba, kwenye mechi ya Euro 2024 hatua ya 16-bora iliyopigwa katika Uwanja wa Merkur Spiel-Arena, Duesseldorf nchini Ujerumani juzi. Ufaransa ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# *Marekani yashiriki uzinduzi Ndondo Cup 2024 nchini*

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani kupitia mradi wa Breakthrough Action, mwaka huu imejiunga na wadau mbalimbali nchini kuandaa Ndondo Cup 2024.

Shirika la Maendeleo la Marekani la (USAID) na Mfuko wa PEPFAR, umeipa shavu Ndondo Cup kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, benki pamoja na kampuni nyingine binafsi.

Lengo likiwa ni kusogeza huduma za afya hasa VVU na chanjo kwa wapenzi na mashibiki wa michuano hiyo inayofanyika kila mwaka Dar es Salaam.

Ujio wa Marekani kwenye Ndondo Cup 2024, unafanywa kupitia Kampeni ya Afya ya Vijana ya Sitetereki, ikilenga wanaume kupambana na VVU.

Kampeni hiyo iliyobeba ujumbe 'Furaha Yangu Chanjo ni Maisha' itabeba mashindano ya Ndondo Cup 2024 yatakayofanyika katika mikoa nane ya Tanzania; Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Kagera, Dodoma, Mwanza na Pwani.

Mashindano hayo yalianza rasmi mwishoni mwa wiki, ambapo ilipigwa mechi ya ufunguzi ya kusisimua kati ya Manzese Warriors na Makuburi FC kwenye Uwanja wa Kinesi uliopo Kata ya Sinza.

Washiriki walipata huduma kamili za afya, ikiwa ni pamoja na vipimo vya VVU na matibabu na huduma za chanjo ambapo mgeni rasmi alifurahishwa na mpango huu wa ubunifu, akiipongeza kamati ya maandalizi na wadhamini kwa kujumuisha burudani na huduma za afya.

"Tumejitolea kubuni mbinu zinazotoa matokeo halisi ya kiafya," alisema Evangelina Chihoma kutoka Ofisi ya PEPFAR.

"Tunaamini kwamba michezo inaweza kuongeza nguvu kubwa katika kuleta mabadiliko ya tabia na kuboresha upatikanaji wa huduma, na tunafurahia kushirikiana na Ndondo Cup na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanikisha mashindano haya."

Lulu Msangi, Mtaalamu wa Programu kutoka USAID, aliongezea, "Tunatumia michezo kuhamasisha Watanzania kupata chanjo na kulinda familia zao."

"Mpango huu wa ubunifu utatekelezwa kwenye ngazi ya kitaifa na jamii, ukilenga kuwafikia vijana wanaoshiriki shughuli za kimichezo kupata elimu na huduma za afya hasa zinazohusu VVU na chanjo. Kwa kuingiza huduma za afya katika burudani, mpango huu unalenga upokeaji wa huduma za afya miongoni mwa wavulana na wanaume kwa kutumia umaarufu wa soka."

# Michezo

Jumatano Julai 3, 2024

Nipashe




De Bruyne: Sijaamua kustaafu UKURASA 22

NJOONI!...



Mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, akipiga hesabu namna ya kuwatoka 'msitu' wa wachezaji wa Ubelgiji kwenye mechi ya Euro 2024 hatua ya 16-bora iliyopigwa katika Uwanja wa Merkur Spiel-Arena, Duesseldorf nchini Ujerumani juzi. Ufaransa ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba: Mukwala, Mulate ni ufunguzi, vyuma vinakuja

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

BAADA ya jana Simba kuwatangaza rasmi wachezaji wawili, straika Steven Mukwala raia wa Uganda akitokea Klabu ya Asante Kotoko ya Ghana na winga, Mzambia Joshua Mutale wa Power Dyanamos, imesema kuwa bado inaendelea na usajili mkubwa inaoufanya, ikitamba kuwa kilichoonekana sasa ni sawa na mvua za rasharasha tu, za masika na kwamba kubwa bado.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema hiyo ni asilimia chache tu ya usajili walioufanya, na wachezaji wanaowasajili wote wanaowatangaza wamefanyiwa tathmini kubwa na benchi la ufundi limeridhika na viwango vyao.

"Ni wachezaji ambao ukiwa nao wanakuhakikisha timu yako kupata ushindi, mfano Mutale akiupata mpira pembeni yeye anakimbilia ndani kwenye lango la mpinzani, hakimbii kama msaidizi wa mwamuzi anayekuwa pembeni tu mwa uwanja, si aina ya wale mawinga ambao wanakimbia ili kwenda kupiga krosi, bali yeye mwenyewe anaingia kusababisha hatari, tumepata mtu, ni kijana mdogo ana miaka 22 tu.

"Tayari yupo nchini anasubiri safari ya kwenda Ismailia kuweka kambi ambayo rasmi tumetangaza leo kuwa ni Julai 7, mwaka huu, ndiyo tutaondoka hapa nchini kwenda kuanza maandalizi ya msimu ujao," alisema Ahmed.

Mutale alitambulishwa juzi usiku, huku Mukwala akitambulishwa jana saa saba mchana.

"Mukwala naye ni chaguo sahihi, ana miaka 24 sasa, huyu kijana ndiye alikwenda kumaliza utawala wa kina Emmanuel Okwi na Farouk Miya kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Uganda, uzuri na yeye ameonekana kufurahia kuchezea Simba kutokana na rekodi nzuri ya wachezaji wa timu hiyo walioichezea miaka ya nyuma, Okwi na Patrick Ochan," alisema Meneja Habari huyo.

Licha ya timu yake kumaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi ya Ghana, Mukwala amemaliza akiwa nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora nchini humo, akipachika ma-

INAENDELEA UKURASA 23

# *Yanga yamletea Aucho mshindani*

### Ni mkata umeme wa kimataifa, yatangaza siku ya...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Yanga iko mbioni kumshusha nchini 'mkata umeme' (kiungo mkabaji) kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Onoya Sangana Charve, anayeichezea Klabu ya AS Maniema, ili kuongeza nguvu kwenye eneo hilo ambalo humilikiwa na Khalid Aucho, huku pia ikitangaza rasmi Agosti 4, mwaka huu kuwa ni siku ya Kilele cha Wiki ya Wananchi.

Japo kikosi cha Yanga kina wachezaji wengi mahiri katika eneo hilo ambao ni Aucho aliyeongezewa mkataba wa miaka miwili hivi karibuni, Zawadi Mauya, Jonas Mkude na Mudathir Yahaya, inataka kiungo mwingine ili kusaidiana na waliopo kwa kile kilichoelezwa kuwa na michuano mingi msimu ujao.

**Taarifa kutoka ndani ya uongozi wa klabu hiyo zinasema Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ameagiza atafutwe kiungo mkabaji mwingine mwenye uwezo kama Aucho kwani akikosekana kutokana na sababu mbalimbali kama vile majeraha, kadi au kufungiwa, pengo lake linaonekana bayana.**

"Tumeona ni kweli, msimu miwili eneo hilo linatuponza, tulifungwa fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na USM Alger ya Algeria kwa sababu tulimkosa Aucho aliyekuwa na kadi, na hatukufanya vizuri dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini hatua ya robo fainali moja kati ya sababu ni kwama hatukuwa na wachezaji wetu nyota wenye uwezo mkubwa akiwamo Aucho kwa sababu mbalimbali, na kuna wakati hapa alikuwa majeruhi, kwa hiyo lazima tupate mtu mwingine," alisema mtoa taarifa wetu.

Alisema, mara nyingi Mudathir anatumika kama mchezaji asiye na namba maalum, anakwenda mbele kusaidia mashambulizi na kurudi nyuma kusaidia kukaba, hivyo tegemeo zaidi kwenye ukabaji ni Aucho pekee.

Mtoa taarifa huyo aliyeongeza kuwa mchezaji huyo amepatikana kwa msaada mkubwa wa Maxi Nzengeli na iwapo mazungumzo yatakwenda vizuri, basi atajiunga na Yanga hivi karibuni.

Akizungumzia kuhusu usajili, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kwa sasa wanachama na mashabiki watapata pia taarifa za klabu hiyo kupitia simu zao za mkononi ambazo si za kisasa kwa njia ya ujumbe mfupi.

"Mpaka sasa tuna vyanzo mbalimbali vya habari kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii ambazo zinatoa taarifa, lakini kwa sasa tumeongeza tena huduma nyingine ya kupata habari zetu, inaitwa Yanga Habari, sasa hapo haijalishi shabiki au mwanachama ana simu janja, au zile zinaitwa 'kitochi' zote watatapata taarifa za usajili wa wachezaji na zingine nyingi kwa njia ya ujumbe mfupi," alisema Kamwe.

Akizungumzia siku ya kilele cha Yanga, maarufu kama Siku ya Wananchi, alisema kutakuwa na mkusanyiko wa matukio ya wiki nzima, ikiwamo kuzindua jezi.

"Tarehe nne ndiyo kilele, na watu wanafahamu ni mkusanyiko wa matukio ya wiki

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >